# *Malkia Wa Sheba*

Sasa tunapokikaribia kiti Chake cha enzi:

2 Baba yetu wa Mbinguni mwenye Neema, tunakuja kwa unyenyekevu katika Uwepo Wako huku vichwa vyetu vimeinamisha na mioyo iliyoinamishwa pia hapa, kwa kuwa tunatambua jambo hili moja: kwamba sisi, siku moja, tutasimama Mbele Zako kutoa hesabu kwa ajili ya maisha yetu, kwa hiyo wakati tukiwa hai na tuna akili timamu, tunatamani kupata amani, na kujua ya kwamba Damu imepakwa kwenye kizingiti cha mlango wa mioyo yetu na juu ya nguzo.

3 Nasi tunasimama kwa uchaji leo mbele Zako kuomba ya kwamba utazifunika dhambi zetu, kutokuamini kwetu, kwa Damu ya Bwana Yesu, na kwenye Siku hiyo tupate kusimama bila makosa wala hatia Mbele za Mungu, tumefunikwa na Damu ya Mwanawe Mwenyewe.

4 Na, Bwana, tungeomba ya kwamba utalibariki kundi hili la watu, ambao wamekusanyika hapa alasiri ya leo si kwa kusudi lingine ila kulitukuza Jina Lako, na kuongeza Kanisani wale ambao wangeokoka, na kufanya yote yaliyo ndani ya uwezo wetu tupate kuuona Ufalme wa Mungu, na kusudi la Mungu likitekelezwa duniani.

5 Wabariki hawa, ndugu zangu, walio hapa jukwaani, wahudumu hawa, wachungaji, wachungaji wa kundi. Tunaomba, Bwana, ya kwamba jambo fulani litafanywa, ambalo litawachochea zaidi ya hapo awali. Jalia Roho Mtakatifu aje miongoni mwetu alasiri ya leo na kufanya mambo mengi sana na kwa wingi kuliko yote tuwezayo kufanya au kuwazia.

6 Nasi tunayaombea, Bwana, makundi yao ambayo yamekusanyika, ya kwamba watavuviwa, nao Wakristo wata—wataazimia zaidi kukuishia Wewe kuliko hapo awali maishani mwao. Na kwa m—mgeni aliye ndani ya malango yetu leo, tungewaombea hasa, ya kwamba wao, pia, waweze kujiunga na ushirika huu mkuu wa waaminio kama hawajafanya hivyo tayari.

7 Nasi tungeomba, Bwana, na tusiwasahau wale wanaopata nafuu, waliofungiwa ndani kwa sababu ya magonjwa na shida, tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa karibu nao. Waponye magonjwa yao na unyoshe mahali pao panapoparuza, Bwana, ili wao, pia, waweze kupiga mbio kwa saburi yale mashindano yaliyowekwa mbele zetu.

8 Tutakapoondoka leo, na twende kwenye makazi yetu, kama wale waliokuwa wakitoka Emau, wakisema maneno haya: “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi

njiani?" Na haya yote yawe kwa utukufu wa Mungu, kwa kuwa kwa unyenyekevu tunainamisha vichwa vyetu na mioyo yetu kama watumishi Wake, katika Jina la Yesu. Amina.

9 Mwaweza kuketi. Nina furaha sana leo kuwa hapa kwenye Maporomoko ya Klamath, katika maskini ukumbi huu wa kupendeza, pamoja na hawa marafiki wa Kristo, na kuendeleza ushirika wetu na Ro—Roho Mtakatifu kwa njia ambayo ametushughulikia na kutufanyia, bila shaka tunathamini baraka Zake zote.

10 Na jana jioni tulipoona wengi wakishuka kuja madhabahuni kuyasalimisha maisha yao kwa Bwana Yesu, jinsi tunavyomshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo! Hilo ndilo kusudi kuu lililotuleta hapa. Kwa kuwa ninaamini katika Injili yote, na uponyaji wa Kiungu, na yote ambayo Kristo alikufa kwa ajili yake, bali kama ukiponywa kwa uponyaji wa Kiungu, siku moja, kama ukiishi muda mrefu vya kutosha, utakuwa mgonjwa tena.

11 Mtu fulani alisema wakati mmoja, kulikuwa na mtu aliyekuwa mkosoaji, aliyeandika katika ki—kitabu, mkosoaji wa dhehebu maarufu la kanisa, naye akaandika katika hicho kitabu ukosoaji wa huduma yangu, naye akasema, "Vema," akasema "kuonyesha ya kwamba. . .Hitimisho nililofikia kuhusu hiyo mikutano lilikuwa hili," kasema, "kamwe hapakuwa na shaka kwamba kulikuwako na nguvu fulani pale ambazo zingefahamu siri ya moyo." Kasema, "Nilikuwa na marafiki pale waliofanyiwa huo upambanuzi," kisha kasema, "walijua hiyo ilikuwa ni kweli."

12 Akasema, "Lakini huo uponyaji, usingeweza kuwa sahihi," akasema, "kwa sababu kulikuwa na mtu aliyeketi kwenye roshani," ambaye alikuwa ni rafiki yake kwenye kanisa lingine, kanisa ndugu, kanisa jirani, "mtu huyo alikuwa na ugonjwa mbaya wa figo ambao alikuwa nao kwa miaka mingi." Kisha kasema, "Ndugu Branham alimwita mtu huyo kwa jina, nasi tulimleta mle kutoka mji mwingine."

13 Kisha kasema, "Alimwambia kuhusu ugonjwa wake mbaya wa figo, na hata mambo fulani yaliyotukia barabarani wakati alipokuwa ameketi katika moja ya zile roshani," na kusema, "tunajua hiyo ilikuwa ni kweli." Kisha kasema, "Mtu huyo alikuwa mzima na mwenye afya kwa yapata miaka mitatu, ambayo hakuwa nayo tangu alipokuwa mvulana, halafu," kasema, "ukamjia tena." Kasema, "Kwa hiyo haungeweza kuwa ni wa Mungu," kasema, "kwa sababu kama Mungu angekuwa amemponya, angekuwa mzima, kwa kuwa mtu akiponywa mara moja, ameponywa."

14 Inaonyesha tu, jinsi ambavyo kama. . .mtu hana budi kukusudiwa na Mungu apate kuamini, la sivyo kamwe hawataamini, kwa vyovyote vile, hawana kitu cha kuaminia.

Mnaona? Hawana tu kina cha nafsi ya—ya—yao. Kama... Nimewajua watu wengi ambao wamewekwa chini ya hema la oksijeni, na kupewa penisilini, na kadhalika, na daktari, na kuponywa kabisa nimonia, tuseme, naye mtu huyo akaondoka hospitalini akiwa mzima kabisa kwa nimonia, halafu juma moja baadaye akafa kwa nimonia. Alishikwa tu na nimonia tena, hivyo tu, bali aliponywa.

15 Halafu tena wakati marehemu, mheshimiwa Ndugu Jack Coe, alipofanyiwa kesi yake, wakati kanisa fulani la kimadhehebu lilipoungana na kafiri kumpiga vita Ndugu Coe huko—huko Florida kwenye kesi yake. Ndipo basi hakimu, akitaka kuonyesha haki, na hata hivyo ni watu wa kanisa, kama gazeti lilivyosema, walikuwa wamemgeuka Ndugu Coe, nao walikuwa wameungana na Joe Lewis, wale wenye mawazo huru, makafiri, huku wakijiita kanisa mashuhuri, bali kwa sababu tu walikuwa wanampinga Kristo sana, na kupinga uponyaji. Lakini inaonyesha jinsi linavyotokea vizuri.

Hakimu akasema, "Bw. Coe, hivi bado unadai ya kwamba mtoto huyu aliponywa?"

Akasema, "Ninadai Kristo alimponya huyu mtoto."

16 Naye akasema, "Alitoa magango yake upande mmoja wa jukwaa mbele ya Bw. Coe, akatembea jukwaani, kisha akamwangukia mama yake, akiwa kiwete." Basi akasema, "Ungeweza kunionyesha mahali popote, kama kuna mtu yeyote hapa anayeweza kunionyesha mahali popote katika Biblia ambapo Kristo aliwahi kufanya ujanja kama huo, nitakuwa tayari kuachana na kesi."

17 Ndipo Kasisi Gordon Lindsay, mmoja wa wavulana wenu wa Oregon hapa, akasimama, akasema, "Ninaweza kutoa hicho kisa." Ndipo Bw. Lindsay akasimulia hicho kisa, akasema, "Usiku mmoja Yesu alikuja akitembea juu ya maji." Kisha akasema, "Petro alipiga mayowe kutoka kwenye mashua, na hao wengine wakasema, 'Ikiwa Wewe ni Kristo, Bwana, niamuru nije Kwako juu ya maji.' Ndipo Petro akashuka kutoka chomboni na kuanza kumwendea Yesu, kama kawaida, juu ya maji, lakini alipoogopa, akazama."

18 Hilo lilitosha, hakika. Unaweza kuponywa dakika moja, na ukawa mgonjwa hiyo nyingine. Unaona? Inategemea imani yako itashikilia kwa muda gani. Nayo imani ndiyo yote ambayo... Uponyaji wa Kiungu na wokovu si kitu ambacho sisi kama watu binafsi tunaweza kufanya, tayari ni kazi iliyomalizika ambayo Kristo alifanya pale Kalvari, ni imani yetu katika kazi hiyo iliyomalizika.

19 Huenda nikawaambia wasikilizaji hawa alasiri ya leo, "Ni wangapi walio Wakristo?" Labda asilimia tisini na tano, ama labda mia moja, wameinua mikono yao, wao ni Wakristo. Mradi tu unaamini hilo, vema, lakini dakika ile unapoanza kuwazia

kwamba sivyo, huo ndio wakati unapoanza kuzama, papo hapo, huo ndio wakati ushuhuda wako ni kinyume. Uponyaji wa Kiungu unadumu mradi tu imani yako inadumu nao, wokovu wako ni vile vile, kwa sababu kila—kila kitu cha Mungu ni kwa imani, wala hakuna kitu cha Mungu kinachoweza kuthibitishwa kwa mambo ya kawaida.

20 Angalia silaha zote za Mungu, ni imani. Silaha za Mungu ni nini? Upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, saburi, imani. Angalieni tu kile kinachoingia katika hizo silaha, kila kitu cha kimbinguni. Huwezi kukishughulikia kwa mikono yako, huna budi kuamini. Hebu shuka uende dukani ukaninunulie upendo wa Kiungu unaogharimu robo, ukaninunulie imani ya thamani ya dola moja. Huwezi kuinunua, ni karama ya Mungu, nawe huna budi kuiamini, huna budi kuiamini. Mradi tu. . .

21 Halafu basi kama ukisema ya kwamba umeokoka, na ungali unayaishia mambo ya ulimwengu, matunda yako yanathibitisha ya kwamba hujaokoka. Unaona? Bila shaka. Daima nimesema ya kwamba mimi ni mkali sana, ninaamini utakatifu, kabisa. Nami nilisema, mimi. . .Lakini kama ukijifanya tu kuvaa kama mtu mtakatifu, ama kutenda kama mtu mtakatifu, hilo halikufanyi mtu mtakatifu. Unaona? Huenda ikawa unaiga tu hilo, lakini kama Roho aliye ndani yako anakufanya uishi hivyo, basi unajua uko sawa, hivyo ndivyo mnavyojihukumu wenyewe, ndipo hamhukumiwi, ama, hamhukumiwi pamoja na ulimwengu, mradi tu umejihukumu mwenyewe kwa maisha ambayo Roho aliye ndani yako anakufanya uishi. Loo, huyo ni Mungu.

22 Sasa, katika mikutano hii, ninii yetu. . .hatuna, kile tunachoita, kuufanya kubwa uponyaji wa Kiungu. Kwa sababu uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo, na kamwe huwezi kulifanya kubwa jambo dogo. Wewe—wewe. . .Uponyaji wa Kiungu ni kitu tu ambacho Mungu alikiongeza Kanisani. Wala hakuna mtu anayeweza kuhubiri wokovu wa nafsi bila kuhubiri uponyaji wa Kiungu kwa ajili ya mwili. Ni kama tu ikiwa mnyama fulani alining'ata pembeni hapa, naye alikuwa tu akikata ubavu wangu kwa makucha yake, hakuna haja ya kuukata tu mguu wake, ama, makucha yake aliyoyaingiza ubavuni mwangu, mgonge tu kichwani, inamwua mnyama mzima.

23 Vema, hivyo ndivyo Kristo alivyofanya wakati alipokufa kwa ajili ya dhambi, aliua kila sifa ya dhambi, mnaona, Yeye aliua kitu hicho chote. Na kabla hatujawa na dhambi yoyote hatukuwa na maradhi, maradhi ni sifa ya dhambi; bila dhambi hawakuwa na ugonjwa. Basi wakati. . .Maradhi ni matokeo ya dhambi, wala huwezi kuishughulikia dhambi bila kuyashughulikia maradhi. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Kwa hiyo unaposimamisha suala la dhambi, unaathiri pia suala la magonjwa, yote yanashughulikiwa, pamoja. Na hiyo ndiyo sababu Kristo alikufa, mtu kamili, mauti

kamili, ufufuo kamili, kwa ajili ya Kanisa kamili, kwa ajili ya Injili kamili. Sawa. Na kwa hiyo, yote yanaambatana pamoja.

24 Sasa, tunaona...Unasema, “Vema basi, Ndugu Branham, huduma yako inajulikana kama uponyaji wa Kiungu.”

25 Hakika, bila shaka. Uponyaji wa Kiungu huvutia. Hiyo... Karibu asilimia themanini na tano ya huduma ya Yesu ilikuwa ni uponyaji wa Kiungu. Mlijua hilo? Kama mzee, marehemu Dk. F. F. Bosworth alivyozoea kusema, “Kamwe humwonyeshi samaki ndoana, unamwonyesha chambo; ananyakua chambo, ndipo ananaswa na ndoana.”

26 Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Watu huja ku—kuona nguvu na miujiza ya Mungu, ndipo wanapoona jambo hilo, wao, kwa kweli Mungu huwashika kwa ndoana kwenye taya papo hapo, maana wanajua ya kwamba kuna kitu halisi.

27 Nilipoenda Bombay, India, na sehemu zingine nyingi...Hao si...Askofu mkuu wa kanisa la Kimethodisti, na hao wengine, walikutana nami kule kwenye...walipokuwa na mashada ya maua na kadhalika yakining’inia nje, wakasema, “Vema, Ndugu Branham, usije hapa ukisema wewe ni mmishenari,” kasema, “tunajua zaidi kuhusu Biblia kuliko ninyi Mayankii mtakavyowahi kujua.”

28 Na hiyo ni kweli, naam. Ni Kitabu cha Mashariki. Vema, ni...Ukienda, ukiwahi kwenda Mashariki na kusoma Biblia, Ni—ni Kitabu kipya kabisa kuliko kile ulichosoma huku Magharibi. Tunajaribu kufanya Kitabu cha Mashariki kilingane na maisha ya Magharibi, huwezi kufanya hivyo. Ile mifano na kadhalika ni mikamilifu kabisa, ingali iko. Nao walikuwa na Biblia miaka elfu mbili kabla hatujakuwa taifa, kwa hiyo haya basi. Mnaona?

29 Walisema, “Tunajua kuhusu Biblia, tunasikia ya kwamba Mungu amekupa karama inayoifanya Biblia hii iishi tena, hilo ndilo tunalovutiwa nalo, si wamishenari,” kasema, “tunao hao chungu nzima hapa. Lakini tunasikia ya kwamba—ya kwamba Mungu amekupa wewe karama ambayo itaifanya Biblia hii iishi maisha Yake tena, Kitabu cha Matendo tena.” Kasema, “Hilo ndilo tunalotaka kujua.”

30 Nikasema, “Yesu Kristo anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele, hiyo ni kweli kabisa.” Nikasema, “Hajabadilika hata kidogo.” Na hapo ndipo Bwana alipoanza kutenda kazi mle ndani.

31 Sasa, mimi...Tuna watu mashuhuri kote...Marekani itahukumiwa kuliko taifa lolote ulimwenguni kwenye Siku ya Hukumu, kwa sababu imekuwa na watu mashuhuri sana ndani yake, katika ardhi yake, katika kuta zake hapa, ndani ya milki ya—yake, kwa sababu kumekuwa na uamsho baada ya uamsho ulioenea kote nchini, na hata hivyo watu wanaendelea kuzama moja kwa moja katika dhambi, wakizidi kuwa wabaya

zaidi kila siku. Mnaona? Kanisa, hata lenyewe, linapoa na kumwacha Mungu. Inasikitisha. Lakini tufanye nini juu yake? Biblia ilitabiri mambo haya yangekuja, na yatakuwa hapa.

Unasema, "Vema, kwa nini unalililia?"

32 Kwa sababu mtu fulani hana budi kukemea makosa, ili kwamba kwenye Siku ya Hukumu, kutakuwako na sauti iliyorekodiwa, hiyo ni kweli, kwamba unajua walijua vizuri zaidi, na yote ya ishara.

33 Si muda mrefu uliopita, tulipokuwa tukija Bombay, nilininii tu. . . Kitu fulani kilinijia moyoni mwangu wakati huo. Nilikuwa nikisoma makala kwenye gazeti ambapo walisema, "Hapana shaka tetemeko la ardhi limemalizika, ndege wanarudi." Yapata siku tatu kabla ya hilo tetemeko kuu la ardhi kuja, kama mlivyosoma kwenye gazeti lenu. . .

34 Mbona, India yote si kama nchi hii, ina. . . nyua zao si waya zilizofumwa kama tulizo nazo, na majengo yao karibu yote yamejengwa kwa mawe wanayoweza kuokota makondeni, nyua zao zimejengwa kwa mawe. Basi hao ndege wadogo wanarudi wakaingia kwenye mawe haya na kutengeneza viota vyao, nayo mifugo alasiri namna hii, wanasimama kwenye kivuli cha kuta hizo.

35 Vema, waliona ya kwamba yapata siku mbili kabla ya hilo tetemeko la ardhi kutokea, maskini ndege wote waliondoka kwenye hayo mawe, wakaacha viota vyao, makazi yao, wakaenda makondeni, wakaishi mitini; ng'ombe na kondoo wasingesimama kuzunguka hizo kuta tena, walisimama nje katikati ya uwanja, wameegemeana. Ndipo tetemeko la ardhi likaja na kuziangusha hizo kuta. Kama hao jamaa wadogo wangalikuwa pale, wangepondwapondwa, ng'ombe wangeuawa, kondoo wangeuawa.

36 Sasa, kama Mungu aliyewaongoza wanyama kuingia safinani angali ni Mungu yeye yule, kwa silika Yeye aliwaongoza mbali na hatari, mbali na kuta hizo zilizokuwa zinaanguka. Vema, kama—kama ndege, na kondoo, na ng'ombe, na wanyama wanaweza kuwa na silika ya kutosha kuongozwa mbali na hatari, ni zaidi sana vipi Kanisa la Mungu linapaswa kuondokea kuta za mambo ya ulimwengu sasa, wakati zikiwa karibu tu kuporomoka? Ondokeni enyi marafiki, mteteeni Kristo, mwaminini Kristo.

37 Sasa, ninaamini ya kwamba huduma hizi tulizo nazo leo kote ulimwenguni, moja tofauti na nyingine. . . Nilikuwa nikimwangalia Ndugu Oral Roberts muda mfupi tu uliopita chumbani, wana televisheni chumbani kwenye. . . waliyokuwa nayo kwa ajili yangu, nami nilikuwa. . . Niliwasikia wakitangaza ya kwamba Oral Roberts. . . Nami nikaenda na kuifungua hiyo televisheni, wakaifungua, ndipo nikamwona Oral akimwombea maskini mtoto mchanga, mgonjwa kutoka

huko Canada, alikuwa na jicho bovu; nami naamini hao wazazi walikuwa Wakatoliki. Naye Ndugu Roberts katika njia yake halisi ya imani, aliupigia mkono wake juu ya huyo mtoto mchanga na kumwombea, maskini mtoto huyo mchanga akaponywa. Sasa, hiyo ni karama halisi ya imani aliyo nayo Ndugu Roberts.

38 Nasi tunajua ya kwamba Ndugu Jack Coe, alikuwa na fuawe ndogo imewekwa karibu na dawati lake, mtu fulani akaja amevaa miwani, angevua hiyo miwani na kuivunja kwa nyundo, na kuitupilia mbali; akiwa na magongo, angechukua magongo yao kwanza, na kuyakatakata, na kuyatupilia mbali, angeteketeza kila daraja.

39 Walikuwa na Jack Coe mmoja tu, mwajua, ulimwengu haungeweza kuwastahimili wawili kwa wakati mmoja. Mungu na aipe raha nafsi yake ya thamani, bila shaka alikuwa ni mtu hodari wa imani. Mmoja wa watu wakuu sana niliowahi kuona maishani mwangu alikuwa Jack Coe. Vema, sasa, na yeye—yeye ameenda Utukufuni leo. Kazi yake ilikwisha, wala Shetani asingeweza kumchukua mpaka kazi yake ilipomalizika.

40 Sasa, sasa, kuna—kuna watu wanaotofautiana mmoja na mwingine, kwa jumla. Na katika huduma ambayo Bwana amenipa, karibu watu hao wote walikuwa wanatheolojia, waalimu mashuhuri na wasomi, yangu sivyo, yangu zaidi sana ni ujumbe wa kinabii. Na jinsi ninavyofundisha uponyaji wa Kiungu ni kazi ya msalabani ambayo imekamilishwa kwa ajili yako, na kama tu utautambua, unaweza kuupokea.

41 Sasa, sasa, Ndugu Roberts na hao watu hodari sana, unasema, "Waonaje huduma yao ikilinganishwa na yako?"

42 Wanatumia Maandiko kwa kuwekea mikono. Sasa, hiyo ni kweli, hilo ni Fundisho la Biblia. Ni wangapi wanaojua hilo? "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Lakini kama mtanivumilia tu kwa dakika moja, ninataka kuwaonyesha hilo halikuwa ni agizo la Mataifa. La, bwana.

43 Yairo alisema, "Njoo uweke mikono Yako juu ya binti yangu, naye ata—atapona." Kiyahudi, Wayahudi daima walikuwa wanawekeana mikono, kila kitu ni kuwekea mikono.

44 Lakini mwangalie Mmataifa, haikuwa hivyo, "Sistahili Wewe uje chini ya paa langu, nena tu Neno, mtumishi wangu ataishi."

45 Naye akageuka, akasema, "Sijapata kuona imani kama hiyo katika Israeli."

46 Hiyo hapo. Tunapaswa kuwa katika kiwango cha juu zaidi kuliko ilivyokuwa. Tunaishi karibu na mwisho wa—wa ulimwengu kuliko tulivyokuwa wakati huo. Njia ya Mataifa ni kuamini Neno, kweli kabisa, kutambua.

47 Mwangalie huyo Mmataifa, alisema, “Mimi ni mtu chini ya mamlaka,” Alikuwa akida, ambayo inamaanisha kwamba alikuwa na watu mia moja chini yake, akida wa Kirumi, naye—naye akasema, “Mimi ni mtu chini ya mamlaka, ninamwambia mtu *huyu*, ‘Nenda,’ naye anaenda; mtu *huyu*, ‘Njoo,’ naye anakuja. Hana budi kuja, yuko chini ya mamlaka yangu. Na hata sikujiona ninastahili kuja Kwako, hakuna yeyote wa taifa langu, nilimtuma Myahudi Kwako.” Kisha kasema, “Mimi. . .Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kunena tu Neno.” Alitambua nini pale? Kwamba kila dhambi, na kila ugonjwa, na kadhalika ulikuwa chini ya mamlaka Yake. “Sema tu, ‘Ondoka,’ nao utaondoka.”

48 Mnaona yale aliyofanya? Sasa, hilo ndilo ninalojaribu kuwafanya Wamarekani waone. Kwamba haininii. . .Si lazima ungojee wakati maalum, ili mwinjilisti fulani apitie hapa, na, ku—kuwaombea, mchungaji wenu ametosha. Kama mchungaji hayupo, jirani yako anatosha; kama jirani hayupo, mumeo au mkeo ametosha; na kama hakuna mmoja wao hapo, inua tu mikono yako, Yeye anatosha daima. Popote tu ulipo, amini, amini, ni kazi iliyomalizika.

49 Na jana usiku, sikuwa nikikusudia kuninii. . .Huo upambanuzi ama karama, hunidhoofisha, hunisumbua sana. Nami nina mwezi mzima wa mkutano moja kwa moja mbele yangu sasa. Halafu basi, ni—nilikuwa nikijaribu kuukwepa kwa siku moja ama mbili usiku, na kwenda tu, nihubiri kwa muda kidogo, kama mngeweza kuvumilia hilo. Halafu mwishoni mwa ibada, Roho Mtakatifu, nilipoanza kuondoka baada ya wito huo wa madhabahuni, Roho Mtakatifu alishuka chini, nililiangalia hilo jengo, hii hapa ile Nuru ikienda kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Mnaona, lilikuwa ni jambo lililokuwa tayari kutukia, na hapo likatukia. Mnaona?

50 Sasa, kwa njia sahihi, kama mngaliweza kulipokea vizuri, wakati huo kama kila mtu humu ndani angaliangalia juu, ingemaliza swali la ugonjwa kwa kila mmoja wenu, kama kila mmoja wenu angaliweza kulipokea. Huyo ni Kristo akijileta Mwenyewe mbele za watu, wapate kujua ya kwamba Yeye hajafa, bali Yu hai milele, Yu hai. Na mradi tu unajua Yule aliyeliandika Neno na kutoa ahadi anaishi papa hapa pamoja nanyi, Yeye ni halisi tu leo katika ahadi Yake, kama alivyokuwa wakati alipokuwa huko nyuma. Hilo linamfanya Yeye yule yule jana, leo, na hata milele.

51 Sasa, Wamarekani wamefundishwa njia nyingi sana mbalimbali, hizo ndizo zinazolifanya gumu. Nenda Afrika, na Congo ya Ubelgiji, au Tanganyika, ama popote unapotaka kwenda, ambako baadhi ya nchi hizo ambazo hazijashindiliwa mambo mengi mbalimbali, mmoja wa wahudumu wetu anasimama na kusema, “Vema, sijui, hiyo huenda ikawa ni telepathia, nisingejipumbaza nayo.”

Wengine wanasimama, "Loo, huyo kweli ni ibilisi, hakuna mtu anayepaswa kujipumbaza na hilo."

Huyo mwingine anasimama, "La, ninaamini ni ya Bwana."

52 Watu watajuaje la kufanya? Ha—ha—hawajui tu jinsi ya kuipokea. Ni ya kimbinguni, ni kuu, wala hawajui jinsi ya kuipokea. Lakini ukiingia mle, hawana yoyote ya mambo hayo. Wanabeba sanamu chini ya mkono wao, iliyonyunyiziwa damu, kitu pekee wanachojua ni mungu wao wa kikafiri. Wanapoona kitu fulani, mungu huyo wa kikafiri hawezi kufanya mambo yoyote ya kimbinguni, basi wanapoona jambo la kimbinguni likitukia, wako tayari kumvunjilia mbali mungu huyo wa kikafiri na kumpokea Kristo.

53 Huko Durban, Afrika Kusini, ambako niliona mwujiza mmoja, kulikuwa na watu wanne jukwaani, ndipo mwujiza mmoja ulipofanywa huko wa hao, niliwaona makafiri elfu thelathini wavaao blanketi wakivunjilia sanamu zao ardhini na kumpokea Kristo.

54 Kesho yake asubuhi, Sidney Smith, meya wa Durban, akaja, akasema, "Ndugu Branham, hebu kidogo, angalia dirishani mwako." Kasema, "Kama unaweza kuisikia . . . "

55 Nikaenda dirishani, na haya hapa yanashuka malori saba makubwa ya kubebea ng'ombe, malori makubwa ya kubebea ng'ombe, yaliyojaa mikongojo, viti vya magurudumu, na fimbo, na kadhalika walizokuwa wakitembelea. Hawana vitu halisi kama tulivyo navyo, ninii tu . . . Ndipo jambo moja tu lilikuwa limetukia, jambo moja tu, ninii tu, ndipo Waislamu elfu kumi wakampokea Kristo wakati mmoja pale, Waislamu elfu kumi waliorekodiwa kwa wakati mmoja.

56 Sasa, waliweka picha hiyo kwenye gazeti hivi majuzi kuhusu Billy Graham na kuhusu Mwislamu huyu akitoa changamoto. Nanyi mliona gazeti hili lingine likitolewa, na kusema, "Kwa nini hamkulitaja hilo?" Mnaona? Vema, wanakosa tu mahali pa oasisi, bali mahali fulani ambapo wangeweza kumshambulia Ndugu Billy Graham, ama kitu kama hicho. Lakini inapofikia uponyaji wa Kiungu, wanajua ni kweli, wanajua nguvu za Mungu, waliziona papo hapo.

57 Na—na kwa hiyo basi, na haya hapa magari haya yote ya kubebea mifugo, na watu waliokuwa kwenye vitanda hivi na machela siku iliyotangulia walikuwa wakitembea barabarani wakiimba katika lugha yao ya kienyeji, "Amini tu, mambo yote yanawezekana, amini tu." Niliketi kwenye dirisha hilo, nami nikalia kama mtoto mchanga, mnaona, kuwaona wakishuka kuja barabarani, mnaona. Tukijua ya kwamba siku moja . . . Nao hata wakiwa katika vita vya kikabila, lakini wote walikuwa mmoja.

58 Nilipata ma—makala yaliyokatwa kutoka kwenye gazeti la Durban yaliyosema kwamba katika muda wa miezi sita baada ya

hapo katika kabila la Shangaan peke yake, ninasahau ni malori mangapi ya mizigo ya—ya risasi, na bunduki, na zana za vita, na kadhalika walizokuwa wamerudisha, na ninii . . . kuvirudisha mahali pake, kwa sababu hao watu walikuwa wameongoka kweli, ha—hawakutaka kujihusisha tena na chochote kibaya. Wao . . .

59 Na sasa hili hapa jambo moja zaidi kabla ya kufunga, samahani kama nimewaudhi, sikusudii kuwaudhi, jambo ambalo siwezi kuelewa huku Marekani ambako tunadhaniwa kuwa wastaarabu, kila mwaka wanawake wetu huvua nguo zaidi kidogo, na hapo walisimama hao wanawake walio uchi, hawana kitu hata kidogo, kitambaa, wamesimama pale na hata hawakujua mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, na mara walipompokea Kristo kama Mwokozi binafsi, walikunja mikono yao wawaondokee watu na kuvaa nguo.

60 Na kama Kristo juu ya mwanamke mwenyeji, kafiri, atamfanya atambue ya kwamba yeye yu uchi, na kwa baadhi ya wanawake wetu wenyewe wa Kipentekoste, wanaodai kuwa na Roho Mtakatifu, huku wakiendelea kujivua nguo hapa nje wapate kutenda kama bingwa fulani wa sinema, ama wengine . . . Siwezi kulielewa. Kuna jambo fulani limeenda kombo mahali fulani, mnaona.

61 Sasa, waweza kuwazia mimi ni mzee aliyechaganyikiwa, lakini ndugu, hiyo ni akili ya kawaida tu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli tu ya Injili, kwa hiyo kuna kasoro mahali fulani, rafiki. Tunachohitaji ni mtu fulani kulisema, mtu fulani kulisimulia, na mtu fulani kuliishi. Sasa, hiyo ni kweli kabisa.

62 Sasa, Bwana na atusaidie. Na kuzungumza hivi, maana ninajua sitaki kuchukua wakati wenu mwingi kupita kiasi, makanisa yenu yatakuwa usiku wa leo. Ninyi wageni, najua, mlikuwa na wakati mzuri mikutanoni asubuhi ya leo, nao watakuwa na ibada usiku wa leo. Nasi tumeuweka wetu alasiri, ili kwamba tusiingiliane na ibada hiyo. Ninataka kuwaombea wagonjwa. Kila mmoja wenu aliye hapa kutoka kwa makanisa yaliyotutembelea, mmekaribishwa mje juma hili. Tunatarajia kuwa na wakati mzuri sana katika Bwana juma hili. Sasa, mara nyingine tena, hebu tuombe kabla hatujalifungua Neno.

63 Bwana Yesu, tunatambua Uwepo Wako, tunajua ya kwamba Wewe upo hapa, na umewakusanya watoto Wako pamoja alasiri ya leo, wanaume na wanawake ambao wangekufa kwa ajili Yako, bure. Watu walio hodari, wanaosimama mimbarani na kuutangaza Ujumbe wa Kristo bila kupatana kwa njia yoyote, hata hivyo kwa upole na utamu. Baba, tunaomba ya kwamba utambariki kila mmoja aliye katika Uwepo wa Kiungu.

64 Sasa, Biblia inasema ya kwamba "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno." Na ninaposoma, alasiri ya leo, somo hili dogo ambalo nimechagua kwa ajili ya ujumbe, ninaomba

ya kwamba utamchukua Roho Mtakatifu, na kutoa kwake muktadha, ambayo ingeleta kweli ya Kristo katika kila moyo, na uponyaji wa Kiungu upate kufikia kila mgonjwa.

65 Na tunapowaombea wagonjwa, naomba ujibu maombi. Na jalia hata kabla mstari haujafanyizwa na wagonjwa kuombewa, Mungu, naomba kwamba katika Jina la Yesu, ya kwamba utawaponya watu kabla ya wakati huo kuja, wapate kujua haliko ndani ya mwanadamu, ni katika nguvu za imani yao kumwamini Bwana Yesu. Tunaomba hayo, katika Jina Lake. Amina.

66 Katika Mathayo Mtakatifu mlango wa 12 na kifungu cha 42, fungu linalojulikana sana kwa wengi wa watu wanaoifuatilia hii mikutano, ningetaka kujaribu kuliendea kwa njia nyingine—nyingine:

> Na *malkia wa kusini atasimama* siku za mwisho *pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu alikuja kutoka pande za* mwisho *za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.*

67 Mathayo 12:42. Unapoenda nyumbani, huenda ukasoma hiyo sura nzima ya Mathayo 12.

68 Sasa, Yesu wakati huu alikuwa akiwakemea watu, kwa sababu hawakuwa wameelewa huduma Yake. Nao walikuwa wakimtazamia Masihi kuja, walikuwa wakimtazamia M—Mkombozi atakayewatoa chini ya nira za utumwa wao. Naye alipokuja, alikuja kwa njia ambayo. . .katika ile siku kuu waliyoishi, mfumo wa kimadhehebu, wa kidini sana ambao ulimwengu uliwahi kujua, walikuwa nao wakati huo; tunajua hilo. Mungu, kupitia kwa Musa, aliyewapa zile Amri Kumi, nao wakachukua Amri hizo na kuziingiza katika madhehebu mbalimbali, na kadhalika, namna hiyo.

69 Lakini kote katika wakati, kulikuwako na wachache waliosalia waliokuwa wameshikilia kweli ya Mungu, kundi dogo tu. Kanisa la Mungu daima limekuwa katika uchache. Ni wangapi wanaojua hilo? Hiyo ni kweli, daima katika uchache. Wakati Yesu alipokuja, kulikuwako na karibu dazani moja, Simeoni, Yohana Mbatizaji, na—na Yusufu na Mariamu, na wachache tu kama hao, walikuwa wameshikilia ile kweli.

70 Sasa, na wakati alipokuja, alikuja kwa njia tofauti sana na vile watu walivyokuwa wakimtarajia kuja, ama, walikuwa wamefundishwa kwamba Yeye angekuja, mpaka alipowachanganya hivi kwamba, hata ha—hawakumtambua.

71 Ninaamini litakuwa ni jambo lile lile atakapokuja tena. Kila mtu ana chati, "Yeye atakuja amepanda farasi mweupe." Huyo mwingine akasema, "La, Yeye anakuja juu ya wingu jeupe." Inaleta tofauti gani mradi tu Yeye anakuja? Mnaona? Mradi tu. . .

72 Kama Yuko juu ya wingu jeupe ama farasi mweupe, sijali, jambo pekee maadamu niko sawa kwenda pamoja Naye wakati huo utakapowadia, hilo ndilo jambo muhimu. Lakini wanatengania hapo, mmoja ataanzisha kundi *hapa*, mwingine kundi *hapa*, kama tu Yeye atapanda farasi mweupe ama wingu jeupe. Kwa hiyo haileti tofauti yoyote, maadamu Yeye yuaja. Na hilo ndilo jambo muhimu, ni kuamini Yeye yuaja.

73 Lakini wakati Yesu alipokuja, Yeye alikuja jinsi hasa Maandiko yalivyotabiri Yeye angekuja, ila tu hayakupatana na mafundisho yao ya siku hiyo. Walimtarajia Masihi kuja . . . Walikuwa wakitazamia Kuja Kwake Mara ya Pili badala ya kuja Kwake mara ya kwanza, hapo ndipo walipochanganyikiwa.

74 Alikuwa akija mamlakani. Walikuwa wakimtazamia achukue fimbo ya chuma na kuyatawala mataifa yote, ndipo alipokuja kwa upole, amezaliwa katika hori, usuli haramu nyuma yake, kama ulimwengu ulivyodhania, akazaliwa katika hori, Mvulana wa kipekee, njia Zake zote zilikuwa za kipekee, akiyararua makanisa, kuyagawanya, na kuwaambia walikuwa wanafiki, na Mafarisayo na—na Masadukayo na hao wote, walihukumu jambo hilo lote, ndipo akasimama hapo peke Yake.

Nao wakasema, "Mbona, tunajua ya kwamba neno lako si kweli." Kasema, "Katika Israeli inahitaji watu wawili kufanya ushahidi."

75 Akasema, "Mimi ni Mmoja, na mwingine ni Baba Yangu atendaye kazi ndani Yangu, kwa hiyo tunao wawili. Na kama sizitendi kazi za Baba Yangu basi msiniamini Mimi, bali nikizitenda kazi za Baba Yangu, wala hamwezi kuniamini Mimi, ziamininі hizo kazi mpate kuokolewa." Mnaona? Mungu alikuwa akishuhudia.

76 Watu wengi wanafuata ishara, si ishara, ni sauti inayoambatana na hiyo ishara. Musa, wakati alipopewa ishara mbili, Mungu alimwambia, "Wasipoisikia sauti ya ishara ya kwanza, basi watasikia sauti ya ishara ya pili." Kila ishara ni ishara tu. Mwanadamu ana karama na kadhalika, lakini angalia kilicho nyuma yake. Shetani karibu anaweza kuiga chochote, yeye ni mwigaji, naye anaweza kuiga. Lakini angalia ni sauti ya namna gani. Inafanya nini? Sauti *ya* ishara.

77 Hebu mtu fulani aje, mkubwa, yale wanayoweza kufanya, na jambo hili lote, usijali hilo. Roho wa Mungu ni Roho mpole, Roho mnyenyekevu, aliyejaa upendo na huruma, akiwatazama watu wote, akiwaleta watu wote wapate kumjua Kristo.

78 Sasa, Yesu alikuwa amekuja jinsi hasa ambavyo Yeye . . . walisema . . . Biblia ilisema angekuja, Naye akafanya vile hasa Biblia ilivyosema angefanya, na hata hivyo, hawakumwamini. Alifanya ishara ya Masihi na kuwaonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, mlango ule ule, nao wakamwita

Beelzebuli, ibilisi, kwa sababu aliweza kuyatambua mawazo yao; nao walidhani ya kwamba Yeye alikuwa ni ibilisi.

79 Sasa, Biblia ilikuwa imewaambia dhahiri, Musa, kiongozi wao waliyemtazamia, aliwaambia ya kwamba "Bwana Mungu wenu atakapowaondokeshea Nabii mithili yangu, na itakuwa ya kwamba yeyote asiyemsikia Nabii huyu atakatiliwa mbali na watu."

80 Sasa, Masihi alikuwa awe Nabii. Na wakati ishara hii ya nabii ilipotolewa miongoni mwao, basi loo, hawakuitarajia hiyo, walimtarajia mtu mwenye fimbo ya chuma ambaye angeweza kutoka na kufanya mambo makuu, na kulipiga taifa.

81 Mnaona, Marekani hakika imezama katika vitu vikubwa na vitu vya kelele, bali Mungu haji katika vitu vikubwa wala vitu vya kelele. Wakati Eliya alipokuwa amerudi pangoni, ngurumo ilipita, Mungu, yeye aliiacha tu ipite, upepo ukapita, walikuwa na upepo wa nguvu ukienda kasi na chochote kile kikipita, bali Mungu hakuwa ndani yake, lakini wakati Sauti ndogo tulivu iliponena, nabii alifunika uso wake na kutoka nje, Yeye akanena.

82 Sauti hiyo ndogo tulivu ndiyo tunayokosa kuisikia, tunatazamia ngurumo na radi, na—na mambo kama hayo, na mihemko. Lakini Mungu . . . Unaweza kudanganywa katika mhemko. Tunataka kudumu na Neno kujua kama tuko sahihi au la, hiyo ndiyo Ramani, dumu na Neno, nalo Neno ni kweli.

83 Nayo Biblia ilikuwa imesema na kutabiri jinsi Yeye angekuja, na wengi wa wale waliokusudiwa, hapo awali, kwa Uzima wa Milele, walimsikia na wakamtambua. Filipo, Petro, wengi wa hao, walipokuja, Yeye angewaambia wao ni akina nani, upesi, wangesema, "Huyo ndiye Masihi."

Lakini Mafarisayo wasingeweza kujibu makusanyiko yao, kwa hiyo iliwabidi kuibandika kitu fulani, nao wakasema tu, "Ni ibilisi."

84 Naye Yesu alikuwa akiwakemea, na kuikemea miji ambayo alikuwa ameifanyia kazi kubwa, kwa sababu kwamba mioyo yao ilikuwa migumu, nao . . . Naye alikuwa akitangaza habari zake katika nyakati zote, Mungu katika nyakati zote, katika kila wakati, amekuwa na ishara na maajabu na mjumbe duniani, katika nyakati zote. Kila wakati uliopata kuja, Yeye alikuwa na mjumbe.

85 Na kama watu waliamini Ujumbe huo, taifa lilifanikiwa, kama halikuamini Ujumbe huo, taifa hilo lilihukumiwa na kuingia katika machafuko. Angalia tu nyuma katika historia ya Biblia na bila shaka utalipata. Kama Mungu alituma Ujumbe . . .

86 Na kwa kawaida Ujumbe hauji na ngurumo kubwa mno, kitu fulani kikubwa, ni kitu kidogo. Hebu mwangalieni Nuhu, yule mlokole; mwangalieni Ibrahimu; angalia tu kote katika Biblia, na hata Yesu Mwenyewe: jina nyenyekevu, duni, lililotengwa,

nyuma Yake, kila kitu. Mwangalieni Yohana: mtu aliyezaliwa nyikani, hana elimu hata kidogo, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo na mwili mzima umejaa manyoya, alionekana kama mmoja wa hawa wadudu hapa waliojaa manyoya, huko nje akihubiri toba, huku akila nzige mwitu na asali. Hilo si ni jambo fulani?

87 Na hawa makasisi mashuhuri, wazuri, wanavyojiita pale, loo, wamefundishwa vilivyo, wangeweza kutamka kila neno la Kiebrania sawasawa, na sarufi yao na theolojia yao ilikuwa kamilifu, naye Mungu akachukua kitu kama maskini mdudu mwenye manyoya timtimu huko nje nyikani na kutuma, na kukihukumu kitu hicho chote.

88 Hata wakati Yesu alipokuja, Yeye alisema, "Hakuna mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama Yohana Mbatizaji." Hiyo ni kweli. Mungu hufanya mambo madogo, lakini yenye nguvu.

89 Sasa, Biblia ilinena, na kusema, ikinena juu ya Yohana kuwa mtangulizi pale, kasema, "Kila mahali palipoinuka patashushwa, kila bonde litainuliwa, milima itaruka kama kondoo dume wadogo, na miti yote itapiga makofi."

90 Ilikuwa ni kitu gani? Maskini mtu mwenye uso uliokunjamana huku amejifunika kipande cha ngozi ya kondoo, nusura awazamishe watu, kwa maji, wakisimama nje kwenye kingo za Yordani, akiyakemea makanisa.

91 Angalieni wakati Yesu alipokuja, walikuwa wamemtarajia Masihi kushuka kwenye ushorobo wa dhahabu, Mtu mzima kabisa mwenye fimbo ya chuma mkononi Mwake, amepanda magari ya farasi, huku amezungukwa na Malaika, mambo makubwa mno ya madoido, naye angeshuka na kuchukua mamlaka, na kuisukumia Rumi nje, na kuteketeza kitu hicho chote, na kuwapa Israeli ufalme. Yeye alikujaje? Mtoto mchanga, Yehova-Mtoto aliyezaliwa katika hori juu ya lundo la samadi. Kweli, hiyo ni kweli kabisa. Kwenye uvundo wa zizi Yeye alishuka, hakuna mahali alipopata kwenda shuleni, ama alipowahi kuingia shuleni, hakuna mahali popote, alienda kila mahali akifanya miujiza na ishara, nao watu wakamhukumu.

92 Wakati alipokuja kubatiziwa huko chini Yordani, mtu wa kawaida tu akitembea kando ya mtaa, ama, kando ya barabara, akashuka akaenda nyikani akabatizwe na maskini mhudumu huyu aliyejaa ndevu huko chini. Mnaona? Mungu hutenda kazi kwa njia Zake Mwenyewe, na—nao watu, huna budi kujinyenyekeza.

93 Mwajua, mambo makuu maangavu ndiyo yanayoyapofusha macho ya watu. Hawa alikuwa akitafuta nuru mpya, akaipata. Biblia ilisema katika siku za mwisho ya kwamba pepo wangekuwa . . . watajigeuza kuwa wahudumu wa nuru. Angalieni dhambi ya kwanza kabisa iliyopata kufanywa,

ilikuwa ni Shetani akitamani ufalme mkuu zaidi, na mwangavu zaidi, jambo kuu, naye akaenda kaskazini na kuanzisha ufalme wake mwenyewe apate kumshinda Mikaeli. Mnaona, daima ni mambo hayo maangavu.

94 Sisi si tumbili, tumbili hutafuta vitu viangavu, hebu tuwe wanaume na wanawake, wenye busara, tuketi chini, tuangalie Injili, tuone inavyosema, kisha tuufuate uongozi wa Roho Mtakatifu. Kamwe hutaweza kumjua Mungu, mpaka Roho Mtakatifu atakapoingia ndani yako. Hiyo ni kweli kabisa.

95 Biblia ilisema ya kwamba "Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu." Kama hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu, bado hujui ya kwamba Yeye ni Kristo; kumbuka hilo. Unaelekea tu kwenye Nuru hiyo.

96 Unaweza kusema, "Mchungaji wangu alisema hivyo." Hiyo ni kweli. "Biblia yangu ilisema hivyo." Hiyo ni kweli. "Mama yangu alisema hivyo." Hiyo ni kweli. "Kanisa langu linaamini ni Roho Mtakatifu." Hiyo ni kweli, lakini wewe je?

97 Kama mtu binafsi, hujui mpaka umempokea. Na unapompokea Roho Mtakatifu, basi wewe ni shahidi ya kwamba Yeye yu hai milele. Sasa, Roho Mtakatifu yuko ndani yako, sasa, basi mwangalie anapotenda kazi. Kama Uhai wa Kristo uko ndani yako, utazaa Uhai Wake ndani yako.

98 "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya." Kazi zile zile, kwa sababu ni Uhai ule ule.

99 Kama uhai katika mti tambaazi wa tikitimaji ukizaa tikitimaji, vema, utazaa, tawi lingine likitokea, litazaa tikitimaji jingine, kila wakati litakuwa ni tikitimaji. Basi iwapo kanisa kweli limetiwa nanga katika Kristo, kila kanisa litaandika Kitabu cha Matendo nyuma yake. Hiyo ni kweli kabisa, kwa sababu la kwanza liliandika Kitabu cha Matendo nyuma yake. Kwa hiyo, haya basi.

100 Naye Yesu hakika alikuwa amewathibitishia ya kwamba alikuwa amewapa ishara ya Masihi, kwamba wakati wa mwisho ulikuwapo kwa ajili yao, nao hawakuamini. Naye alikuwa akiwakemea na kuwaambia. Ndipo akarejea nyuma basi, nyuma katika kifungu kinachotangulia hiki, katika kifungu cha 41, Alipendelea pale, ama kurejea, hasa, kwa Yona, "Katika siku za Yona."

101 Sikuzote nilimhurumia Yona, watu wengi sana wanamhukumu Yona. Mbona, Yona alikuwa ni nabii, alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu. Unawasikia wakisema, "Loo, yeye ni Yona." Ninaamini ya kwamba Yona alifanya yale hasa Mungu aliyomwambia afanye.

102 Siamini ya kwamba mtumishi yeyote wa Mungu, akiongozwa na Roho, anaweza kutoka nje ya mapenzi ya Mungu, kwa sababu mradi tu anaongozwa na Roho, hayo ni

mapenzi ya Mungu. Wakati mwingine hufanya mambo ambayo hata yeye mwenyewe hajui yale anayofanya, wala hatambui ni kwa nini anayafanya, bali ni Mungu akiifanya kote kwa manufaa. "Kila kitu hufanya kazi kwa manufaa ya wale wampendao Mungu," yalisema Maandiko.

103 Naye Yona, hakika, Mungu alimwambia aende Ninawi, lakini *kwa namna moja au nyingine*, pasipo hu—huyo nabii kujua, alichukua merikebu isiyofaa, akashuka kwenda Tarshishi, nimeninii. . ., ama, kuelekea njia hiyo. Bahari ikaja, nayo mawimbi yakaanza kuvuma, na pepo zikavuma. Sikuzote nilimhurumia Yona. Mnajua, walimfunga mikono na miguu yake, wakamtupa nje ya meli, ndipo samaki mkubwa akammeza.

104 Basi mtu yeyote anajua ya kwamba wakati samaki anapokula chakula chake cha kutwa, ama, mlo wake, anashuka chini na kupumzisha pezi zake chini ya maji, chini ya ziwa. Hebu mlishe samaki wako wa dhahabu, uone kitakachotukia, watashuka moja kwa moja chini ya mtungi huo mdogo na kupumzika. Anazungukazunguka majini mpaka anapata chakula chake, akiisha kula, anashuka na kupumzika.

105 Sasa, nyangumi huyu mkubwa, dhoruba baharini ilikuwa imekuja, naye Yona alikuwa ametupwa nje, ndipo Mungu akamtuma nyangumi huyu aende kumchukua Yona, naye akammeza Yona na kushuka chini chini ya bahari apate kupumzika. Naye huyo hapo Yona, amefungwa mikono na miguu, chini ya bahari, katika tumbo la nyangumi.

106 Ati unazungumza kuhusu dalili? Yona alikuwa nazo, a—alikuwa na haki ya kuwa na dalili. Angalieni hapo, kama aliangalia *huku*, lilikuwa ni tumbo la nyangumi, kama aliangalia *huku*, lilikuwa ni tumbo la nyangumi, kila mahali alipoangalia, palikuwa ni tumbo la nyangumi.

107 Sasa, hakuna mtu hapa ndani katika hali hiyo, yupo, dada? Usingekuwa katika hali hiyo, ama wewe hapo, ama yeyote wenu. Hakuna mmoja wenu aliye katika hali hiyo. Sasa, yeye hakuninii. . .Hakuna mtu aliyewahi kuwa mahali hapo alipokuwa Yona: mikono yake ilikuwa imefungwa, miguu yake ilikuwa imefungwa, alikuwa katika tumbo la nyangumi, labda kilindi cha mikono ishirini baharini, na kwenye bahari yenye dhoruba. Unanena kuhusu dalili? Kweli alikuwa nayo. Lakini mnajua yale aliyosema? "Ni ubatili udanganyao, sitaitazama tena, lakini mara moja tena nitalitazama hekalu Lako takatifu."

108 Kwa nini? Wakati Sulemani alipoliweka wakfu hekalu hilo, aliomba huko juu, naye akasema, "Kama watu Wako wakiwa katika shida mahali popote, na kuangalia kuelekea hekalu hili, basi sikia kutoka Mbinguni, Bwana." Naye alikuwa na matumaini katika kile o—ombi la nabii lilichokuwa, kwamba—kwamba angesikiwa kutoka Mbinguni. Naye akakataa

kuangalia dalili za tumbo la nyangumi, akaangalia tena kuelekea kwenye hekalu.

109 Huwezi kumficha mtakatifu kutoka kwa maombi, sijali uendako. Ni. . . Unaweza kumwekea hali yoyote, wale wana wa Kiebrania katika ile tanuru ya moto, Danieli katika tundu la simba, popote pale, mwaminio halisi hushikilia maombi hayo, sijali kinachotukia, yeye hushikilia maombi hayo.

110 Mnajua, katika. . . Mnajua kilichotukia? Mungu alimchefua nyangumi huyo tumboni mwake, ndipo a—akamtapika ufukoni. Sasa, kama Mungu angejibu maombi ya Yona chini ya hali hizo, akiangalia kwenye hekalu ambalo mwanadamu alijenga, lile hekalu ambamo mtu aliomba, hekalu ambamo kulikuwa na kiti cha rehema kilichofunikwa na—na damu ya kondoo, ni zaidi sana jinsi gani atafanya leo, tunapoangalia mbali na dalili zetu, hali yetu ya ulemavu, kansa yetu, uvimbe wetu ama chochote tulicho nacho, ama dhambi yetu, na kukiangalia Kiti cha Enzi cha Mungu, ambapo Yesu anasimama kwenye mkono wa kuume wa Ukuu akiwa na Damu Yake Mwenyewe kutuombea tunapokiri?

111 Sahau dalili zako, kama wewe. . . mradi tu unauangalia mkono wako na kusema, "Umepinda," daima utapindika. "Ninakataa kuuangalia, tena, ninalitazama hekalu Lako takatifu, Ee Bwana." Ninakwambia, kitu fulani kitakuwa kigonjwa, Shetani atakuwa, unapoanza namna hiyo. Ninawatakeni mwone jinsi Mungu alivyofanya jambo hili halisi sana.

112 Halafu, tunaambiwa ya kwamba Waninawi walikuwa waabudu sanamu, tena waliabudu wanyama; ibada zote za sanamu huabudu wanyama. Halafu basi, tunaona ya kwamba—ya kwamba mungu wa—wao wa baharini alikuwa ni nyangumi, kwa sababu alikuwa ndiye mkuu wa bahari, na kazi yao huko Ninawi ilikuwa ni wavuvi. Na hapa watu wote walikuwa huko nje, maelfu yao, m—mji mkubwa kama Portland, Oregon, nao wote walikuwa huko nje kwenye mashua zao wakivua samaki, basi huyu hapa mungu wao anakuja, mungu-nyangumi akaingia, akautoa ulimi wake, ndipo nabii akatoka moja kwa moja kwenye ubao wa kushukia.

113 Hakika, wangesikia ujumbe wake, mungu-nyangumi alikuwa amemtema nabii. Bila shaka. Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo, huenda ikawa ni rahisi, bali Yeye anajua jinsi ya kufanya hivyo, Yeye anajua jinsi ya kuifikia moyo wa watu.

114 Nyangumi akafungua kinywa chake, ndipo huyo nabii akatokea, mungu wao, naye akasema, "Msipotubu, katika siku arobaini mahali hapa patazama!"

115 Moja kwa moja katika Maandiko tunayosoma hapa alasiri ya leo, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa . . . "

116 Basi, angalieni kile walichouliza hapo kwanza, walisema, “Utuonyeshe ishara, Bwana,” hao Mafarisayo wakamwambia, wakasema, “utuonyeshe ishara.”

117 Akasema, “Ki—kizazi kibaya na cha zinaa kinatafuta ishara, wala hakuna ishara watakayopewa ila ishara ya Yona. Kwa maana kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku.”

118 Sasa, ninyi watu wenye nia ya kiroho, fungukeni, angalieni jambo hilo, angalieni hilo, msilisome tu mkaliruka moja kwa moja, acheni Roho alishike kwa ajili yenu. Angalia: Ni kizazi cha aina gani kilichokuwa kikitafuta ishara? Kizazi hiki, hiki ni kile kizazi kiovu na cha zinaa ambacho kingetafuta ishara kila mahali, kila ishara ndogo wanaitafuta. Kasema, “Hakutakuwa na ishara, ila ishara ya Yona.”

119 Yona alikuwa ni ishara ya nini? Ufufuo. Ule ufufuo, hicho ndicho kitu tunachoona sasa, ishara ya ufufuo. Yesu yu hai, hajafa, Yuko miongoni mwetu, akifanya jambo lile lile alilofanya wakati huo, hiyo ndiyo ishara ambayo kizazi hicho kingepokea.

120 Unasema, “Loo, Yeye alikuwa akizungumza juu ya kizazi hicho cha wakati huo.”

121 La, bwana, angalia ishara walizopokea kutoka Kwake, alikuwa akizungumza juu ya kizazi hiki, “kizazi kiovu na cha zinaa.” Angalieni hapa sasa katika nchi yetu, uzinzi ni kama Sodoma na Gomora, bila shaka ndivyo ulivyo, na unaongezeka kila siku.

122 “Kizazi hicho kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara, nao wataipata.” Aliahidi wangeipata, wangepata ishara ya kweli kutoka Mbinguni. Linganisha hilo na siku za Sodoma, “Ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Natumaini mnalipata hilo. Mnaona? “Watapewa ishara,” Yeye alisema. Neno la Mungu liko kwenye alama kila mahali katika Biblia.

123 Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Mwangalieni yule Malaika kule chini kwa Kanisa teule, kwa yale aliyofanya; mwangalieni Yesu, yale aliyofanya katika kizazi Chake; angalieni hapa chini kwenye kizazi hiki, kile anachofanya sasa. Watapokea ishara, bali hawataiamini, haya basi, bali ilikuja vivyo hivyo.

124 “Kizazi kibaya na cha zinaa kitatafuta ishara.” Nao wataipata, watapewa. “Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku.”

125 Lakini ufufuo utakuwa ndio ishara, na ishara ya ufufuo imepewa Kanisa katika siku hizi za mwisho. Malaika wa Roho Mtakatifu mi—mikutanoni, akionyesha mambo yale yale, akifanya mambo yale yale kote nchini, akithibitisha ya kwamba Yesu Kristo amefufuka katika wafu yeye yule jana, leo, na hata milele. Hicho ndicho kizazi ambacho kingeipokea.

126 Ndipo anakuja kwa yule malkia, malkia, tunamwita Malkia wa Sheba, "Malkia wa Kusini," Yeye alisema hapa, kasema, "atasimama katika siku za mwisho na kukihukumu kizazi hiki. Atafufuka katika siku ya mwisho," hiyo ni pamoja na kizazi cha siku za mwisho, "atasimama pamoja nao na atawahukumu, kwa sababu alitoka pande za mwisho za dunia kusikia hekima ya Sulemani, na hata hivyo, nawaambia ya kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani."

127 Sasa, hebu na tumchukue maskini huyo malkia katika siku za Sulemani, na tusikilize kwa makini. Sasa, wasomi wote wa Biblia wanajua ya kwamba siku za Sulemani zilikuwa ni wakati wa ufanisi sana wa—wa Waisraeli. Huo ndio wakati ambao hawakuwa na vita vyovyote kwa ajili ya chochote, walijenga hekalu, na mataifa yote, baada ya Daudi, walikuwa wamewaogopa Israeli, nao wakawaletea mambo makuu, na utajiri, na nguvu, na jeshi lenye nguvu, hakuna mtu aliyewasumbua.

128 Na ndipo walikuwa, Mungu akawapa karama. Mungu hutoa karama katika vizazi vyote, karama ya Uwepo Wake. Sasa sikilizeni, ndipo tunaona ya kwamba Sulemani, baada ya kupokea karama hii ya upambanuzi, iliwekwa katika matendo, nao watu kutoka kila mahali wakamwamini. Sasa, vipi kama wangaliikataa karama hiyo? Mbona, wangekuwa—wangekuwa ni nchi iliyopotea. Lakini waliiamini, kila mmoja aliiamini, haidhuru Sulemani alifanya nini, wangali walidumu nayo. Waliamini ya kwamba alikuwa ni mtumishi aliyetumwa kutoka kwa Mungu.

129 Loo, vipi kama kanisa la Kikristo usiku wa leo, vipi kama kanisa la Kikristo leo lingeweza kuamini Karama ambayo Mungu aliwatumia? Roho Mtakatifu. Vipi kama wangempokea? Vipi kama madhehebu yote yangeunganika kwa Roho Mtakatifu, wakati Israeli walipounganika kwa Sulemani akiwa na karama hiyo? Roho Mtakatifu ni Karama kwa kanisa, nalo kanisa linaikataa na kuifungia nje kwa mafundisho yetu, na theolojia zetu, na kadhalika. Kanuni zetu za imani za kujibunia, tunamfungia Kristo nje moja kwa moja, hatumruhusu Roho Mtakatifu kuingiea, hakuna miujiza, hakuna kupiga makelele, hakuna kunena kwa lugha, hakuna sifa za Mungu.

130 Vema, kama Roho Mtakatifu alifanya hivyo katika Kitabu cha Matendo, atafanya jambo vivyo hivyo leo hii, kwa sababu Kitabu cha Matendo si matendo ya mitume, ni matendo ya Roho

Mtakatifu *ndani ya* mitume. Na Huyo ni Roho Mtakatifu yeye yule Kanisani siku hizi, angetenda vivyo hivyo na kutoa matokeo yale yale. Kwa nini ukubali kibadala wakati anga zimejaa nguvu halisi za Kipentekoste? Haitubidi kuwa na kibadala, tunaweza kupata kilicho halisi. Ninajua ni kweli, ndugu yangu, dada yangu, ni kweli, sasa, matendo ya Roho Mtakatifu.

131 Angalieni katika malkia huyu—huyu sasa, ama, Sulemani, hasa, kwanza, tunaona ya kwamba katika siku za huduma yake, watu wote walikusanyika kumzunguka, kumzunguka Sulemani. Na kila mtu alizungumza . . . Hakukuwa na mtu aliyemsengenya, kila mtu alikuwa upande wake.

132 Sasa, vipi kama kanisa lote la Kikristo leo lingekusanyika kumzunguka Roho Mtakatifu? Hakuna mtu anayesema, "Ni ulokole." Hakuna mtu anayesema Hivyo, kwamba sivyo. Kila Mmarekani angesema, "Loo, jamani! Katika taifa letu tumempokea Roho Mtakatifu." Vipi kama Rais wetu mpendwa sana Eisenhower, na wa—wa—wagombea wote, na kadhalika, wa uchaguzi huu, na watu wote walikuwa tu katika nia moja, nao wangekuwa wakizunguka-zunguka wakisema, "Loo, tumebarikiwa sana, tumebarikiwa sana! Roho Mtakatifu ametuzuru, Naye yuko miongoni mwetu." Naam.

133 Angalieni, niliposhuka kwenye chombo kule chini, chombo anga huko—huko India, wao walisema, "Hatutaki kujua theolojia yako, hatutaki kukusikia ukisema wewe ni mmishenari. Tunasikia ya kwamba Mungu amekupa karama ya kuifanya Biblia iishi tena, tunaitaka hiyo." Jambo ndilo hilo.

134 Loo, ndugu! Kama Kanisa lote la Mungu lililokombolewa lingesimama katika nguvu za Roho Mtakatifu, mataifa yangeliogopa taifa hili. Wana mabomu ya atomiki sasa, nao watailipua vipande vipande moja ya siku hizi, nanyi mnajua hilo. "Mbingu zitawaka moto," alisema Petro, "na nchi itateketea kwa—kwa joto kali," na kadhalika, tunajua inakuja. Lakini vipi kama sisi, kama . . .

135 Watu siku hizi, wakijaribu kuchimba waingie ardhini wapate ki—kimbilio la bomu, kuingiza serikali huko Kentucky mahali fulani katika moja la hayo mapango. Sasa wana bomu ambalo hata hawawezi kujificha pangoni, ukiingia kina cha futi mia moja na sabini na tano ardhini, ama kama ulikuwa umelitengeneza kwa chuma ngumu tupu, futi mia tano ardhini, mtikiso wake ungeua kila . . . ungevunja kila mfupa mwilini mwako, bila shaka ungevunja, utoboe shimo ardhini maili mia moja na hamsini mraba, futi mia moja na hamsini, kina cha futi sabini na tano ardhini.

136 Utayaepukaje? Vema, nitawaambia sasa hivi, Kanisa linalo kimbilio, halijatengenezwa kwa chuma ngumu, limetengenezwa kwa manyoya, chini ya mbawa Zake Kanisa litadumu, nalo

litainuliwa juu Utukufuni, mbali na mambo ya ulimwengu. Hakika.

137 Loo, laiti taifa lingesikiliza tu na kupokea na kukusanyika kuizunguka hiyo Karama, huu ungekuwa ni wakati wa ufanisi mkuu sana. Hiyo Karama ni Roho Mtakatifu ambaye Mungu alimtuma tena. "Tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba Yangu, ngojeni katika mji wa Yerusalemu, hata mtakapovikwa uwezo utokao Juu."

138 Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu."

Wanasema, "Vema, hiyo ilikuwa tu kwa ajili yao."

139 Kweli? Yeye alisema, "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Hiyo Karama ni kwa yeyote atakaye, anaweza kuja. Na kwa Wamarekani waombao, na maskini wazee hawa wa kale waliojitokeza wakipiga vita vizuri vya imani na kulijenga taifa hili juu ya kanuni za Biblia, na watoto wao ambao wamemshikilia Mungu, ambao wameleta uamsho ambao umeletwa Marekani.

140 Lakini wako katika uchache, hao wengine, nguvu za Kikomunisti makanisani, nanyi mnaona mkutano huu mkubwa kuhusu hawa wahudumu, na kadhalika, katika matendo haya makuu ya kanisa hapa, hata wakibeba kadi za Kikomunisti mifukoni mwao, viongozi wa makanisa haya ya kimataifa, na kadhalika, yote yamejaa upotovu. Haina budi kuwa hivyo, kwamba hakuna mwamba mwingine wala msingi mwingine ila Yesu Kristo. "Juu ya mwamba huo nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda." Amina! Hilo ndilo wazo.

141 Kulikuwako na malkia, ama, Sulemani, watu wote wakikusanyika kumzunguka. Mbona, habari zilisambaa kila mahali. Vema, kupitia tu nguvu ndogo za kanisa, habari za Roho Mtakatifu kushuka hapa na kufanya mikutano mikubwa zimewaita wahudumu hawa kote ulimwenguni, kila mahali, kutoka tu kwa nguvu hizo ndogo. Anafanya nini? Kuwatoa Wateule, kuwatoa watoto wa Mungu kutoka . . . "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu." Wanakuja kutoka kila mahali, wakimjia Bwana, Ujerumani, kutoka Uswisi, kutoka Afrika, kutoka India, kutoka Asia, kote ulimwenguni wanakuja. Mioto ya uamsho imewashwa juu ya karibu kila kilima.

142 Watu, walio Wateule, hao wengine wakiwadhihaki, wakiwaita watakatifu wanaojibingirisha na walokole, hilo halimaanishi jambo moja. Lakini ninii . . . mjue yakini ya kwamba ni ku—kusudi la Mungu kwamba wangewahukumu, ili

Yeye apate kuhukumu jambo hilo. Bila shaka. Wasiponinii... Wakiwahukumu, wanamhukumu Yeye, "Kwa kuwa kadiri mlivyomtendea aliye mdogo kuliko wote wa hao ndugu Zangu, mlinitendea Mimi, yeyote wa hawa waniaminio Mimi. Na ishara hizi zitafuatana na hao waniaminio Mimi." Hivyo ndivyo mnavyojua. Sio kukiri kuamini, bali "Ishara nizifanyazo, watazifanya pia. Hilo litakuwa ni thi—thibitisho, sauti kwa huduma yao kwamba wanasema kweli."

143 Enyi wanaume kwa wanawake, amkeni mwone ukweli kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Tuko chini ya vivuli vya rehema Yake sasa hivi, bali siku moja tutakuwa chini ya vivuli vya hukumu, kwa sababu tumevikataa vivuli vya rehema. Kimbilieni kwenye Mwamba.

144 Halafu, nini? Angalieni, watu wote walikusanyika karibu na Sulemani, ile karama ilikuwa kubwa, ilifanya mambo makuu. Hawakuwahi kuona kitu kama hicho, walijua ilibidi itoke kwa Mungu. Upambanuzi kama huo, kamwe hawakuona kitu kama hicho. Wapita njia wote, wangetaka kupitia na kumwona Sulemani, wanataka kuiona.

145 Mbona, Nehru, na wengine, na Khrushchev, na hao wengine, wasingekuwa wakija kwenye taifa hili kuona tu barabara nzuri tunazopaswa kuzimiliki, wasingekuwa wakitaka kuona tuna ikulu ya aina gani, utajiri tulio nao, na jinsi mashamba yetu, ni kiasi gani cha kilimo, ama kadhalika, wasingekuwa wakija kuona hayo, kama sote tungekusanyika karibu na Roho Mtakatifu, wangekuwa wakiona njaa sana kwa ajili ya Mungu, wangemwogopa sana, kwa sababu wanajua ya kwamba Mungu anadhibiti kila chembe ya dunia.

146 Naam, hilo ndilo tunalohitaji siku hizi ni—ni wanaume na wanawake kukusanyika kuizunguka Karama ya Mungu, Roho Mtakatifu. Naye Roho Mtakatifu akitenda kazi ndani yao, akionyesha Uwepo Wake pamoja nao, kusudi wapate, watu, wasioamini wengine, wapate kuona kwamba ni Mungu.

147 Sasa, tunaona ya kwamba wapitaji walipata habari za Sulemani, ndipo sifa zake zikaenea kote ulimwenguni, kisha zikashuka kotekote, Biblia ilisema, hata pande za mwisho za dunia. Sasa, huko kulikuwa ni sehemu za mwisho kabisa za dunia iliyojulikana siku hizo. Na kama utaangalia, ni mbali sana kutoka Palestina kushuka kuvuka Jangwa la Sahara, kufikia mahali alipokuwa huyo malkia, Malkia wa Sheba.

148 Sasa, hebu tuwazie, kila mtu aliyepitia, angepitia karibu na maskini huyo malkia, mwajua, nao wanasema, "Vema, sisi ni wasafiri, tumekuwa huko katika nchi *fulani-fulani*. Loo, laiti ungaliizuru Palestina. Wao ni watu hodari sana, wote wana nia moja, taifa zima linanawiri katika utajiri. Nao wana mtu huko juu aliye na karama kutoka kwa Mungu wao, ambapo mtu

huyo anatenda tu kama vile Mungu wao angetenda, endapo Yeye angekuwa amesimama pale."

149 Mnajua, imani chanzo chake ni kusikia, unaona. Na maskini malkia huyo angesema, "Unajua nini kuhusu hilo?"

150 Loo, ndipo jamaa mwingine akaja, "Naam, mimi . . . Maskini Malkia, tumepitia hapa, nasi tumekuwa safarini, misafara yetu pamoja na ngamia. Na—nasi tulipitia Misri, tukapitia katika nchi zote, ndipo tukafika Palestina, aisee, wana Mungu mwenye nguvu huko juu, Mungu aliye hai. Loo, tuna miungu nchini mwetu, bila shaka, bali wao wana Mungu anayetenda kazi ndani ya watu Wake, Yeye ni Mungu halisi, laiti ungalimwona. Hata walimchukua mtu huyu Sulemani, na kumfanya mfalme wao. Na loo, Mungu wao ana nguvu, laiti ungalimwona."

151 Mnajua, imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno. Kama mtu ana chochote kumhusu Mungu, anaposikia kazi za Mungu, ataanza kuona njaa. Akaanza kufikiria kufanya safari ndogo. Lakini anatarajia hii . . .

152 Sasa, yeye aliishi katika nchi ya kikafiri, tunajua, alikuwa ni kafiri, mpagani, yeye mwenyewe. Lakini hebu na tuchukue mchezo mdogo wa kuigiza sasa. Ningewazia sasa, yeye katika hadhi yake, kabla hajaweza kuondoka nchini, ingembidi kushauriana na kanisa lake na kasisi wake mpagani, endapo angeweza kwenda.

153 Kwa hiyo, ninaweza kumwona akienda kwa kuhani wake, naye akasema, "Baba mtakatifu, ni—nimesikia habari kuu za Waisraeli, ya kwamba Mungu wao huko juu amemtia mafuta mmoja wa ndugu za—zao, naye ni mtu mashuhuri, ambaye anaonyesha maajabu, na ishara, na hekima, na anaweza kuyatambua mawazo ya watu, na mambo makuu anayofanya huko juu."

154 Ninaweza kumsikia huyo kuhani mpagani akisema, "Ewe mtoto wangu, unajua wewe ni malkia? Wewe ni mfuasi wa kanisa hili, kanisa la taifa hili kuu ambalo wewe ni malkia wake? Je, ulijua nyanya wa nyanya wa nyanya wa nyanya yako, na wote kote chini walikuwa malkia kabla yako? Je, ungeliaibisha kanisa lako na watu wako kwa ku—kuhudhuria mkutano wa kilokole kama huo? Mbona, kama miungu waliwahi kufanya jambo lolote, miungu wetu wangelifanya hivyo kanisani mwetu." Kama huo sio msimamo siku hizi, kamwe sikuujua. Naam, bwana.

155 "Mbona," akasema, "lakini sikiliza, nasikia, ya kwamba—ya kwamba Yeye si Mtu fulani ambaye—ambaye tunazungumza habari zake. Sasa, umezungumza juu ya sanamu hizi hapa tunazozitumikia, wala sijawahi kuona moja ya hizo ikitenda chochote maishani mwangu mwote. Nawe unaendelea kusema kwamba hizo ni nini, na kile zitakachofanya, na kile zikachotenda, na kile zilichofanya, sijawahi kuona

msogeo mmoja wake. Jambo pekee nililo nalo ni maneno machache tu hapa ambayo nimekuwa nikisoma juu yake. Lakini wananiambia ya kwamba Mungu wao yu hai. Ninataka kuona kitu halisi."

156 Hiyo ndiyo njaa ya kila moyo wa mwanadamu, wanataka kuona kitu halisi. Wanajua wametoka mahali fulani penye giza, nao wanaingia humu, na kurudi kwenye ile nchi tena wasiyoijua. Wanatafuta wapate kitu fulani ng'ambo ya pazia, hicho ndicho alichotamani.

157 Vema, ninaweza kumsikia huyo kasisi akimwambia sasa, "Binti, ukienda kule, tutakufukuza kanisani. Tutaondoa tu jina lako moja kwa moja kwenye kitabu, wala hutakuwa—hutakuwa mfuasi wa kanisa hili tena."

158 Lakini mnajua nini? Kama njaa ya Mungu ikiingia katika moyo wa mwanadamu, hakuna kitu ulimwenguni kitakachowazuia, hiyo ni kweli, wakati moyo unapoanza kuona njaa. Daudi alisema katika Biblia, "Kilindi kinapoita kilindi."

159 Sasa, kama kuna kilindi kinachoita, hapana budi pawe na kilindi cha kuuitikia. Mnaamini hilo? Sasa, vinginevyo namna hii, ikiwa kabla ya kuwa . . . Vema, nilisoma siku moja hapa miaka michache iliyopita gazetini, kuhusu mvulana mdogo akila vifutio vya penseli shuleni. Mwalimu angempa penseli nyingine, akala kifutio chake. Ndipo mama yake akamwona siku moja huko nje akila pedali ya baiskeli, kwenye . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ilibidi iwe sa—salfa ipate kuitikia shauku hiyo. Mnaona ninalomaanisha? Vinginevyo, kabla hapajakuwapo na kiumbe, hapana budi kuwe na Muumba wa kuumba hicho kiumbe.

160 Basi mradi mko hapa leo, ninyi watu mlio wagonjwa, mkitafuta uponyaji wa Kiungu, kwa sababu mnaamini ya kwamba kuna Mungu anayeweza kuwaponya wagonjwa hiyo inaonyesha kuna chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani kwa ajili ya uponyaji. Kwa kuwa mnamtaka Mungu zaidi, ni kwa sababu kuna chemchemi mahali fulani ambapo mnaweza kumpata Mungu zaidi. Kilindi kinapoita kilindi, hapana budi pawe na kilindi cha kuitikia wito huo.

161 Sasa, maskini malkia huyo, aliposikia kuhusu Mungu aliye hai aliyekuwa akiishi pamoja na watu Wake, ilisababisha kiu. "Heri wao," alisema Yesu katika Mathayo 5, "wenye njaa na kiu ya haki, maana watashibishwa."

162 Kuna jibu unapoona kiu, kuna kitu cha kukata kiu hiyo. Kanuni zetu za imani, madhehebu yetu kamwe hayatakidhi kiu hiyo, huna budi kupata ukweli wa Mungu aliye hai, na njia pekee utakayofanya hivyo, ni kujazwa na Roho Wake, Huko ndiko kukatwa kwa kiu hiyo. Yeye ndiye Sehemu iridhishayo kwa Kanisa Lake, Yeye Ajitoshelezaye kwa Yote, ambaye huridhisha kila shauku. Mtu anapoyaacha mambo ya ulimwengu

na kumjia Kristo, yeye hupata ule utoshelevu wote katika Kristo, anapompata Kristo.

163 Sasa, ndipo akaanza kuona kiu, naye nanii, bila shaka kasisi alimwambia asingeweza kwenda. Lakini, mwajua, kuna jambo fulani kulihusu, kama mtu anataka kumpata Mungu, hakuna kitu kitakachowazuia kufanya hivyo.

164 Sasa, maskini mama huyo alikuwa na vizuizi kadhaa. Na kila mtu anayejaribu kumjia Kristo atakabiliwa na vizuizi, viko kila mahali. Hebu anza tu siku moja, uone. Anza matembezi ya karibu zaidi na Mungu, uone kitakachotukia, jaribu tu, ibilisi yuko mlangoni kukuzuia kwa kila njia.

165 Sasa, jambo la kwanza, yeye alikuwa ni malkia, naye alikuwa na safari ndefu, ilimbidi kuliacha kanisa lake, ilimbidi kumwacha kasisi wa—wake, ilimbidi kuliacha kanisa lake, lakini Yesu alisema ya kwamba, "Yeyote asiyemwacha babaye, mama, mume, mke, watoto, na kadhalika, na kunifuata Mimi, hastahili kuwa mwanafunzi Wangu." Ni kuacha, kujitolea, kusalimisha.

166 Unasema, "Vema, mimi ni . . . mimi . . . Mwajua, mimi ni mfuasi wa vilabu fulani, mimi ni mfuasi wa vyama hivi, nasi sote tunaninii . . . "

167 Huna budi kuacha kila kitu, huna budi kufanya chaguo lako sasa. Je, uko tayari kuacha *kila kitu* upate kumfuata Yeye? Mungu akianza kuweka kiu moyoni mwako, utaacha kila kitu ulimwenguni. Niliondoka kwa baba na mama yangu mwenyewe, nyumbani. Nina mke na watoto watatu wanaoketi moja kwa moja huko nje sasa, kama wangeniambia, "Hakuna kuhubiri tena," ningeondoka moja kwa moja kutoka nyumbani, naam, bwana, kadiri ninavyowapenda, niwafie papa hapa kwa urahisi, lakini Kristo ndiye yote.

168 Yeye ndiye lengo langu, nami . . . kusudi langu Kwake ni kutoa kila kitu nilicho nacho kumfuata Yeye, kama ninaitwa mshupavu wa dini, kama ninaitwa mponyaji wa Kiungu, mtakatifu anayejibingirisha, chochote kile. Siyajali mambo ya ulimwengu, wala siamini Mkristo yeyote huyajali, tunataka kumfuata Kristo. Hilo ndilo lengo langu, kumfuata Yeye, kumwinua. Hilo ndilo tunalohitaji siku hizi, ni watu walio tayari kujitolea.

169 Sasa, maskini huyo malkia alikuwa na mawazo mazuri, ningetaka mwone, alisema, "Sasa, sijawahi kuona jambo hili, sijui lolote kulihusu." Kwa hiyo, ningewazia jambo la kwanza maskini huyo malkia alilofanya lilikuwa ni kujinunulia Biblia, apate kusoma na kujua. Akasema, "Sasa, kama ni kujifanya kwa namna fulani, hakutakuwa ni kulingana na Biblia, Biblia yao, lakini kama Biblia yao imebashiri jambo kama hilo, basi litakuwa ni kweli."

170 Sasa, hivyo ndivyo Wakristo wanavyopaswa kufanya. Unapokuja kwenye mkutano, usilaumu, kwanza yachunguze

Maandiko. Yeye...Vipi kama wangalikuwa—vipi kama wangalikuwa waaminifu namna hiyo kwa Yesu?

171 Kasema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi, na ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele. Mnafikiri mna Uzima wa Milele, Nayo yananishuhudia Mimi." Hiyo ni kweli, hakika.

172 Aliwaambia Mafarisayo, makasisi hao mashuhuri wa siku hiyo, kasema, "Mnaweza kuangalia jua, kumetanda, mnasema, 'Kesho kutakuwa na dhoruba, na kama ni kweupe kesho, kutakuwa na kianga.'" Kasema, "Enyi wanafiki! Mnadhaniwa kuwa makasisi, nanyi mnaweza kuyatambua mambo ya ulimwengu vizuri zaidi kuliko mnavyoweza kutambua ishara za wakati."

173 Kama hiyo si kweli siku hizi! Kila mtu anazingatia ni nani atakuwa rais. Mimi pia, lakini inaleta tofauti gani? Ninataka kujua ni nani atakayekuwa Mfalme wa Umilele, Kristo. Hilo ndilo jambo muhimu. Ninataka kujua kuhusu taifa langu, ninavutiwa nalo, mimi ni Mmarekani, ninavutiwa na taifa langu, lakini, ndugu, hilo na liwe la pili, Mungu wangu ndiye wa kwanza. Naam, bwana.

174 Lakini jambo ni kwamba, wanalichukua taifa, mambo ya ulimwengu, "Ni nani atakayekuwa, ni nani atakayecheza mchezo huu pamoja na bingwa *fulani-fulani* wa sinema?"

175 Watu wengi, watu wengi siku hizi, washiriki wa kanisa, Wapentekoste, Wabaptisti, Wapresbiteri wanaweza kukwambia mengi zaidi kuhusu maisha ya sinema kuliko wanavyoweza kukwambia maisha ya Biblia. Watoto wengi zaidi wanaweza kukwambia kuhusu Davy Crockett, ama—ama *Gunsmoke*, ama baadhi yao, kuliko wanavyoweza kukwambia kuhusu Yesu Kristo, ni kwa sababu hivyo ndivyo wanavyofundishwa nyumbani mwao. Halafu mnazungumza juu ya uhalifu wa vijana? Ni uhalifu wa wazazi na uhalifu wa kanisa. Kweli kabisa. Uhalifu wa makasisi wa kuhubiri Neno, naye Mungu akitenda kazi pamoja na kanisa, akilithibitisha Neno kwa ishara zinazofuata.

176 Anania na Safira walikuwa wakiishi kanisani, kwa mlo wa kanisa wala kamwe hawakukemewa na kuambiwa dhambi zao, kwa sababu wao ndio watoaji kuliko wote walioko kanisani. Baadhi ya Anania wenye kazi kubwa wanaweza kuchangia dola elfu tano kwa mwaka, angeweza kunywa pombe, kuvuta sigara, kucheza kamari, kufanya uzinzi, naye anaweza kuwa shemasi wakati uo huo. Ndugu, ninakwambia, wakati Roho wa Mungu anapoingia kanisani, angekirarua kitu hicho na kukipasua, kama alivyofanya alipokuja wakati ule mwingine hekaluni, wabadilishaji pesa.

177 "Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wasiowapenda walio

wema, wakaidi, wenye kujivuna, wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake, hao nao mjiepushe nao." Ninanukuu Maandiko, Timotheo wa Kwanza 3.

178 Sasa, unapoona mambo hayo yakitukia, na kujua hiyo ndiyo saa tunayoishi, uaminifu ambao kanisa linapaswa kuwa nao, na hata hivyo ni wa ajabu sana. Ukishuka chini hapa sokoni, ama ninii, ama, uende usiku wa leo kwa chakula cha jioni, nao wakuandalie bakuli la supu, huku buibui mkubwa akiwa ndani yake, vema, ungetaka kushtaki kampuni hiyo, bila shaka, nzi yuko ndani yake, ungeninii, mbona, ungemwita maskini huyo mhudumu na kumkemea kwelikweli, na hata hivyo utatembea moja kwa moja, uchukue theolojia ya kujibunia, na kuishindilia kooni mwako, "Jiunge na kanisa, hilo tu ndilo unalopaswa kufanya."

179 "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kamwe kuingia katika ule Ufalme." (Shughulikia hilo. . .?. . .) "Na ishara hizi zitafuatana nao baada ya wao kuzaliwa mara ya pili." Mnaona? Hivyo ndivyo Yesu alivyosema. Hilo huleta alama ya kutofautisha Kanisani, ishara na maajabu ya Kristo aliyefufuka aliye hai, akiishi ndani ya Kanisa. Hawalitaki siku hizi.

180 Maskini malkia huyo alilitaka. Lakini jambo la kwanza alilotaka kujua, "Je, lilikuwa ni la Kimaandiko au la?" Alisoma Maandiko yote. Ndipo akasema, "Nitafanya jambo lingine, mimi ni malkia, na kama ujumbe huo ni wa kweli, nitauunga mkono." Naye akawapakia ngamia dhahabu, na manemane, na uvumba, na namna zote za mavazi ya thamani, na kadhalika. Akasema, "Kama ni kweli, kama Mungu huyo ni Mungu halisi, basi nimemalizana na kitu hiki ambacho nimekuwa nikikitumikia, nami nitakiunga mkono kwa kila kitu nilicho nacho." Huo ndio msimamo.

181 Sikilizeni, Mungu hajali sana pesa zako, bali anataka umwunge mkono kwa yote uliyo wewe, hataki asilimia kumi ya pesa zako, kadiri anavyotaka muda wako, kipaji chako, ushuhuda wako, na yote uliyo wewe yakabidhiwe mikononi Mwake, kusudi aweze kukutawala. Anataka kuwa Bwana wako, sio tu Mwokozi wako, bali Bwana wako, ubwana, kukutawala. Naye. . .

182 Naye akasema, "Nitaiunga mkono ikiwa ni ya kweli, kama si kweli, ninaweza kuzirudisha pesa zangu nyumbani." Hilo ni jambo zuri, la busara kwa Wamarekani wengi kusikiliza, nafikiri hivyo siku hizi, pia. Mipango ya kila namna, na kuiunga mkono, na kulaani kitu kile kile unachoamini. Hiyo ni kweli. Mnatoka nje, na kuunga mkono wahubiri wa redio na kadhalika. . .

183 Sihukumu jambo hilo, sina kipindi cha redio, kamwe sikusudii kuwa nacho. Inaweza kuwa ilikuwa kwenye televisheni? Hakika. Hivi ningalikuwa na majengo, na makanisa, na kadhalika? Niliyahukumu, nikayakataa. Ninataka kuwa

mnyenyekevu, ninataka kufikia mahali fulani, hata ninaweza kwenda mahali popote, chini ya hali yoyote, na kuhubiri popote Mungu anaponiongoza kwenda bila masharti, bila kitu hata kidogo, niwe tu huru kufanya na kusema yale Roho Mtakatifu asemayo niseme, hilo ndilo kusudi langu. Naam, bwana. Nidumu nalo, niongozwe tu na Roho Wake.

184 Vipi kama ingenibidi kupata dola elfu kumi kwa siku? Vipi kama ingenibidi kupata dola elfu moja kwa siku? Mnafikiri ningeweza kuwa huku kwenye Maporomoko ya Klamath? La hasha, Nisingeweza. Bila shaka si lazima niwe na chochote, cha kutosha tu kuwalisha watoto wangu, Mungu hushughulikia hilo, kwa hiyo hicho tu ndicho kinachohitajika. Kwa hiyo haya basi, hakuna msaada na mambo kama hayo. Nami ninaamini ya kwamba Mungu huwapa wahudumu vipindi vya redio na televisheni, ninaamini hilo kwa moyo wangu wote, bali Yeye hakunipa mimi.

185 Sasa, jambo ni kwamba, kama unaunga mkono kitu chema, lakini kwa nini uunge mkono kitu kinachohukumu Pentekoste, na uponyaji wa Kiungu, na nguvu za Roho Mtakatifu, na kuzidhihaki, nawe unageuka, na kumwacha mhubiri wako mwenyewe kwenye redio afe kwa njaa, na imbidi kukatiza kipindi chake, nawe uunge mkono kitu kama hicho? Silielewi. Nami najua maelfu wanaofanya hivyo. Ningeunga mkono kile hasa nilichoamini, na kile nilichowazia, ningekaa mwaminifu kwake mpaka nife, naam, bwana, kwa kila kitu, si pesa zangu tu, bali nafsi yangu, ujuzi wangu, ushuhuda wangu, uwepo wangu, ninii yangu. . . kila kitu nilichoweza kufanya, ningekiunga mkono.

186 Maskini malkia huyo alikuwa na wazo lile lile, si ajabu atasimama katika siku hii ya mwisho na kukihukumu kizazi hiki leo. Naam, alikuwa akienda kuisaidia kwa yote aliyokuwa nayo, aliweka dhahabu yake na kadhalika.

187 Sasa, jambo la pili, ilimbidi kusafiri mbali sana kumsikia mtu huyu, ambaye amezungumziwa sana. Sasa, ilimbidi kuvuka Jangwa la Sahara. Mnajua ilimchukua muda gani kufanya hivyo? Ilimchukua yapata miezi mitatu, siku tisini, naye hakuja kwa Kadilaki iliyoyoyozwa, la, alikuja juu ya mgongo wa ngamia. Hiyo ni kweli.

188 Si ajabu atakihukumu kizazi hiki, watu hata hawatavuka barabara kusikia ujumbe kama huo, kumwona Roho wa Mungu akitenda kazi na kufanya maajabu, wataketi kwenye baraza zao za mbele na kuikosoa, waende mahali pale na kuihukumu, naye alikuja kutoka pande za mwisho za ulimwengu juu ya mgongo wa ngamia, ikambidi kusafiri usiku.

189 Jambo lingine, angalieni kile kilichomkabili safarini mwake, wana wa Ishmaeli walikuwa jangwani siku hizo. Walikuwa ni majambazi, huku naye akiwa na pesa hizo zote, akivuka jangwa,

maskini askari wachache, akiwa na wasichana wachache kama walinzi, matowashi wanne ama watano wamesimama karibu naye, na kusafiri huko nje pamoja na kundi hili kubwa la Waarabu wepesi waendao kasi kwa farasi, wanaopitia jangwani kule, nao angeweza kuwanyang'anya kila kitu alichokuwa nacho, wawaue, na kuwaacha wamelala huko.

190 Lakini mnajua jambo fulani? Unapokuwa na njaa moyoni mwako kwa ajili ya Mungu, hatari hata haikuzuii. Unaendelea tu kusonga mbele, ukipanda juu. Hakuna kitu kitakachotutenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo. Hiyo ni kweli, unaendelea kusonga mbele. Aliendelea tu mbele, kamwe hakuwazia juu ya kifo.

191 Kwa vyovyote vile, kama una njaa kwa ajili ya Mungu, ibilisi ataweka kila kizuizi awezacho njiani mwako, bali Kristo atakiondoa njiani, utembee tu katika Nuru, kwa kuwa Yeye yuko Nuruni. Endelea tu kusonga mbele, naye Mungu atakufanyia njia, Yeye aliahidi kufanya hivyo, Naye atafanya hivyo. Hiyo ni kweli.

192 Akaanza, akawapakia ngamia wake, akaweka zawadi zake zote humo, akaanza kuvuka jangwa, labda akisafiri usiku, kulikuwa na joto sana. Miale ya moja kwa moja ya lile—lile jua katika Jangwa hilo la Sahara, karibu iivishe nyama moja kwa moja kutoka kwenye mifupa yako. Naye huyu hapa akalivuka. Kwa nini? Siku baada ya siku, juma baada ya juma, siku baada ya siku, mwezi baada ya mwezi, akisafiri kupitia jangwani juu ya maskini ngamia hawa wa kale kutoka oasisi moja hadi nyingine, akiwa na kiu sana ya maji, ulimi wake ukining'inia, midomo imekauka, wanaume wake wote wakitembea, wakati wowote wangeweza kuibiwa au kuuawa, haileti tofauti yoyote, ameshika njia aone kama jambo hili ni kweli ama si kweli.

193 Basi wazieni, papa hapa katika mji huu, wafikirie watu siku hizi, mahali hapa pangeweza kuwa pamejaa na kusongamana, uwanja umejaa kabisa, watu wameinua mikono yao hewani, wakimsifu Mungu wanapoona ishara kuu na maajabu yakitendeka, maajabu, miujiza, Maandiko yenyewe yakitimizwa, ishara ya ufufuo kwa kizazi ki—kibaya na cha zinaa. Lakini watafanya hivyo? Si ajabu atasimama katika siku za mwisho na kukihukumu kizazi hiki, kama Yesu alivyosema.

194 Sasa, tunaona, hatimaye akawasili malangoni, salama. Naye alipofika . . . Sasa kumbukeni, watu wengi huja kwenye mkutano kama huo, kama wataona mwujiza fulani wa Mungu ukifanywa, ama ukitendwa, watasema, "Vema, nitakwambia nitakalofanya, nitaingia tu, nami nitaketi chini, na iwapo mhubiri huyo atasema jambo moja ambalo sikubaliani nalo au kanisa langu halikubaliani nalo, nitasimama moja kwa moja na kuondoka." Hiyo inaonyesha ukosefu wa elimu, hivyo ndivyo hasa. Kwanza kabisa hiyo inaonyesha malezi mabaya.

195 Sasa, akaingia, si kukaa na kuona kama mchungaji alisema lolote, Mchungaji Sulemani alisema jambo fulani ambalo hakukubaliana nalo, ama kama kanisa lake, alijua ya kwamba kanisa lake halikukubaliana na hilo, bali alikuja kuketi chini, kuyachukua Maandiko, na kukaa mpaka atakaposhawishika kwa njia moja ama nyingine. Hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Yachukue mambo yanayodaiwa kuwa ni ya Mungu na uyajaribu kwa Maandiko kuona kama ni ya Kimaandiko; endapo ni ya Kimaandiko, yako sawa.

196 Huyu hapa anaingia sasa, naye anapakua mizigo yake yote kutoka kwenye ngamia, anapiga maskini mahema zake huko nje nyuani mwa ikulu, naye atakaa tu mpaka atakaposhawishika. Laiti Wamarekani wangekuwa na wazo kama hilo.

197 "Sijali yale mchungaji asemayo, yale John Jackson asemayo, ama yale dhehebu langu lisemayo, nitakaa mpaka nitakaposhawishika kabisa kama ni kweli ama si kweli. Nami nitailinganisha na Maandiko, neno baada ya neno, ukurasa baada ya ukurasa, nami nitaona kama ni kweli ama si kweli." Alikaa mpaka aliposhawishika, ili aweze kujua.

198 Sasa, hebu tumchukue asubuhi ya kwanza. Vema, ninasikia nyimbo zote zikiimba, kengele zikilia, ndipo—ndipo Sulemani akatoka akaja mimbarani, kwenye hukumu yake, kiti chake cha enzi, akaketi, Mchungaji Sulemani. Kanisa likaimba nyimbo, kisha ba—baragumu zikapigwa, na vyombo vya muziki vikapigwa, ndipo kusanyiko lote likaja. Ninaweza kumwona maskini malkia huyo akiketi kule nyuma, akasema, "Nitaangalia tu sasa nione kitakachotukia."

199 Huyu hapa mtu fulani anakuja, na muda si muda mwajua, akasema, "Sasa nitaona kama ni kweli ama si kweli." Naye akaiangalia, akasema, "Nimesikia, sasa, Mungu huyu ni Mungu anayefanya mambo haya, Nitaona kama Roho huyo wa Mungu yuko ndani ya mtu huyu, huyu mtumishi Wake."

200 Basi mtu wa kwanza alipokuja, Sulemani kwa nguvu zake kuu za upambanuzi, aliipambanua kikamilifu na kumwambia. Loo, jamani! Maskini moyo wa huyo malkia ukaanza kudunda upesi. Siku baada ya siku, na wakati baada ya wakati, lilitukia.

201 Hebu tuseme, hakupata, bila shaka, lakini hebu tuseme tu alipata kadi ya maombi, bali hakuitwa kwa muda mrefu, lakini baada ya kitambo kidogo, wakati wake ukafika wa kuja mbele ya Sulemani. Nayo Biblia ilisema ya kwamba hakuna kitu alichofichwa Sulemani, lakini alimfunulia mambo yote aliyopaswa kujua, akamwambia habari zake.

202 Basi alipoona jambo hili, alisema, "Sasa, naona ikifanya kazi kwa wengine, sijui kama itafanya kwangu. Mimi, kwa namna fulani, ninaamini ya kwamba hiyo ni kweli. Nimejitolea, nimetoka mbali sana nami nitakwambia nitakalofanya, nitaamka nione kama itafanya kazi kwangu."

203 Kwa hiyo akapanda kule juu, naye Sulemani akamwambia mambo yote, Biblia ilisema, "Hakuna alichofichwa Sulemani." Kupitia kwa roho ya upambanuzi, karama ya Mungu, alitambua kila kitu ambacho yeye. . .alichopaswa kumwambia. Nalo lilimridhisha hivi kwamba, alitoa zawadi zake zote kwa kanisa, kwa hiyo huduma.

204 Naye akasimama, na hivi ndivyo alivyosema: "Heri watu walio pamoja nawe, wanaokaa pamoja nawe, wanaokuhudumia, sikuzote wako pamoja nawe, kwa kuwa macho yao yanaiona hii wakati wote."

205 Si kwamba tu watu na kadhalika wamebarikiwa, bali wamebarikiwa wale wanaoona hili likifanywa siku baada ya siku. "Heri watu wanaoambatana nawe wanaoona mambo haya yakifanyika mkutano baada ya mkutano, wakati baada ya wakati. Ni heri jinsi gani!"

206 Naye akaona utukufu wote na Mungu, naye akawa mwongofu, naye Yesu akasema, "Yeye atasimama katika siku za mwisho na kukihukumu kizazi hiki kuwa kimekosa, kwa sababu alikuja kusikia hekima ya Sulemani, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani."

207 Hebu niwaambie alasiri ya leo, enyi marafiki: Hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani, Roho Mtakatifu, Mwenyewe, yupo hapa, Wakala wa Mungu, Yesu aliyefufuka katika umbo la Roho, Mungu amemtuma tena kukaa katika Kanisa Lake, kuwa pamoja nasi, kutenda kazi, na—na kutubariki, na kutupa Uwepo Wake, na kufanya kazi alizofanya. Loo, laiti tungaliweza tu kulinyakua! Laiti mngaliweza tu kulishika!

208 Ni kitu gani kilichomfanya maskini malkia huyo. . .? Katika kufunga, hebu niseme jambo hili, jambo fulani tu linakuja niani mwangu: Sababu ya yeye kusema hivyo na sababu ya kufanya hivyo, ni kwa sababu kwa mara yake ya kwanza aliona kitu halisi, kitu halisi. Aliona kitu ambacho hakingeweza kuelezewa na akili ya mwanadamu, kilikuwa ni cha kimbinguni. Aliona kitu ambacho alijua kwamba kilikuwa halisi.

209 Hadithi ndogo, vema, ama, si hadithi, ni ukweli. Mimi, kila mtu anajua kwamba ninawinda. Ni—nimewinda, mama yangu ni nusu Mhindi wa Cherokee, na mimi—mimi—mimi ninawapenda Wahindi, ninapenda kuwinda, wongofu wangu kamwe haukuniondolea hilo, ninawinda Afrika, Asia, kila mahali; mimi si mwuaji, bali mwindaji. Kwa hiyo ninapenda. . . Mimi ni mhifadhi, nilikuwa—nilikuwa afisa wa uhifadhi mwaka baada ya mwaka, miaka saba Indiana, nami na—naamini katika kuhifadhi wanyama pori. Ninaamini kuwa huko mwituni, kuwa peke yangu, kuna kitu kulihusu.

210 Nilikuwa nikiwinda kwenye Misitu ya Kaskazini, nami. . . nipate kuwa peke yangu. Huko ndiko Biblia yangu ya kwanza ilikotoka, ningeweza kusikia upepo ukivuma kupitia kwenye

miti, nikaona mti ukifa kisha ukaishi tena, niliona ua likianguka katika msimu wa kupukutika mwakani na kuchipuka katika majira ya kuchipua, nikajua kulikuwa na Mungu mahali fulani.

211 Niliangalia utomvu ukisimama kwenye mti mnamo Septemba, Agosti na Septemba, kamwe hakuna upepo baridi uliowahi kuupiga, lakini kabla upepo baridi haujapiga mti huo, ni kitu gani? Utomvu huo huingia chini kwenye mizizi na kujificha wakati wa baridi kali, usipojificha, utakufa katika majira ya baridi kali. Halafu majira ya kuchipua mwakani, huu hapa unarudi ukileta matofaa tena, ukizaa.

212 Ni akili gani inayoelekeza huo kwenye mizizi hiyo? Niambieni. Tia maji kwenye ndoo, kisha uyaweke juu ya nguzo, uone kama yatashuka chini ya nguzo. La hasha, bila shaka hayatashuka. Akili fulani huuingiza chini. Mungu yuko katika maumbile kila mahali, akifanya kazi katika maumbile, na hiyo ilikuwa Biblia yangu ya kwanza.

213 Nami nilikuwa nikienda kuwinda pamoja na jamaa fulani, Bert Call, mke wangu hapa alijua. . . anamjua vizuri. Na kwa hiyo, tulikuwa, tukienda kule mwituni kuwinda, naye alikuwa mmoja wa wawindaji wazuri sana niliopata kuwinda nao. Yeye pia alikuwa nusu Mhindi. Wala kamwe hukuwa na wasiwasi kuhusu kumpoteza, ange—angeingia, alikuwa sawa, alijua mahali pake. Tena alikuwa mwenye shabaha sana, mmoja wa walio wazuri sana niliopata kuona. Wala kamwe. . . Wakati mwingine ukimpeleka mtu mwituni, hujui kama utamwacha, na ikubidi kuendelea kumwangalia, na kumtafuta, atapotelea mahali fulani, lakini kamwe si Bert, mwache tu peke yake, alikuwa sawa.

214 Nasi tulipenda kuwinda pamoja, tulifahamiana. Alikuwa ni jamaa mzuri, lakini katili sana niliyepata kumwona maishani mwangu; jamaa huyo alikuwa dhalimu kwelikweli. Ati asiye na huruma? Sijawahi kumwona mtu asiye na huruma hivyo, alikuwa akiwaua watoto wa kulungu kiholela apate tu kunifanya nijisikie vibaya. Naye angepiga risasi. . . Mwajua, kulungu mdogo ni mtoto mdogo wa kulungu, ninyi watu wa Oregon mnajua jinsi walivyo, naye a—angewapiga risasi kusudi tu. . .

215 Sasa, ni sawa kumchukua mtoto wa kulungu, Ibrahimu alimchinja ndama na kumlisha Mungu. Hiyo ni kweli. Ni sawa kumwua mtoto wa kulungu kama sheria inasema auawe, wao ni wahifadhi, wanajua ni yupi anayeweza kuuawa na asiyeweza kuuawa. Lakini basi, kama. . . Lakini sio kuua tu kundi lao ili kuwa katili, huo ni ukatili.

216 Na kwa hiyo yeye, siku moja nilipanda kwenda kumwona, nasi tulikuwa tukienda kuwinda, naye alikuwa amejiundia namna fulani ya filimbi ndogo aliyoifanya ilie kama mtoto mdogo wa kulungu akimlilia mama yake. Nami nikawazia. . . Nikasema, "Bert, hutaitumia hiyo!"

"Loo," akasema, "Mhubiri, wewe ni mwoga kama kuku, rudia fahamu yako."

Nami nikasema, "Bert, usifanye hivyo."

"Loo," akasema, "endelea. Hivyo ndivyo mlivyo ninyi wahubiri," kasema, "ninyi ni waoga kupindukia. Naam, endelea!"

217 Tukaenda kuwinda asubuhi hiyo, nasi...huo msimu ulikuwa umeendelea sana, na kulungu walikuwa adimu, maana bunduki ya kwanza inapoanza kufyatuliwa, wanaingia mafichoni kule, kwa sababu kuna uwindaji mwingi. Daima tunachukua sambusa na chupa ndogo ya themosi iliyojaa chokoleti moto, maana inatoa lishe na joto, upesi, kwa mwili; kama ungejidhuru mwenyewe, ama chochote kile, ingekuwa ni kuchukuliwa.

218 Nao kulungu walikuwa adimu sana, tulitembea tangu yapata mapambazuko mpaka yapata saa tano na nusu, wala hatukuwa tumeona mkondo mmoja, yapata inchi nane ama kumi za theluji ardhini, hali nzuri ya hewa ya kufuatilia. Tulikuwa tumepitia kwenye mifune mikubwa, na kupanda kupitia sehemu za miti migumu, na kuendelea hadi kwenye mibetula hiyo mingine, na kadhalika, na miti ya kijani kibichi, wala hatukuona chochote, si hata mburuzo.

219 Tukafika kwenye uwazi mdogo yapata ukubwa wa jengo hili, ukumbi huu, naye Bert akainama tu chini namna *hii*, akaanza kuingiza mkono kwenye shati lake. Nilidhani alikuwa anataka kutoa chakula chake cha mchana, nasi tungekula chakula cha mchana, na, kwa kawaida, ndipo tutengane adhuhuri, ndipo mmoja anaenda njia moja, na mwingine nyingine, kisha turudi kambini usiku.

220 Naye alikuwa akinyosha mkono *hapa* ndani, nikaanza kuninii, kushusha bunduki yangu, nikaanza kutoa chakula changu cha mchana, naye alipotoka, alikuwa na maskini filimbi hii, ndipo akanitazama kwa macho yake yaliyoonekana kama ya mjusi. Nami nikawaza, "Hutafanya hivyo, Bert."

221 Ndipo akachukua hiyo filimbi ndogo, akaipiga, ilisikika kama tu mtoto mdogo wa kulungu, mmewasikia, wakimlilia mama yao. Basi—basi akapiga filimbi hii, kisha akaniangalia na kidogo akacheka. Nikashangaa, upande wa pili tu wa huo uwazi, jike kubwa zuri sana likasimama.

222 Loo, alikuwa ni mnyama mwenye sura nzuri, niliona hayo macho makubwa mno, ya hudhurungi, hayo masikio makubwa yakiinuka juu. Nikamwangalia. Alikuwa nini? Alikuwa ni mama, mnaona, na mtoto mchanga alikuwa hatarini, naye akaanza kuangalia huku na huku, "Yuko wapi mtoto huyo?"

Ndipo akaniangalia tena namna hiyo, nami nikasema, "Atafanya hivyo, kwa vyovyote vile."

223 Nikamwona akivuta nyuma ule wenzo kwenye hiyo ya .30-06, mlenga shabaha hodari, kisha akaipiga tena, akayanyosha hayo masikio makubwa. Sasa, hiyo si kawaida kabisa ya kulungu jike kufanya hivyo katika msimu wa kuwinda, wakati huo mchana. Naye akaingia moja kwa moja kwenye uwazi huo, akiangalia huku na huku akimtafuta huyo mtoto mchanga, mahali alipokuwa. Ndipo alipoanza kuinua kichwa chake, huyo kulungu jike akamwona.

224 Vema sasa, kwa kawaida wao, kile tunachoita, linawatisha, mnaona, wao—wao wanaogopa sana, wanatoroka, bali si yeye, akatupa hayo masikio makubwa, hayo macho makubwa ya hudhurungi yakaangalia chini kule, ambako yule mwindaji, kilele cha kofia yake kikitokeza. Nami nikamwona akilenga bunduki hiyo, akaweka hiyo alama ya kulenga moja kwa moja kwenye moyo wake mwaminifu, nikawaza, "Ee Bert, unawezaje kufanya hivyo? Unawezaje kumwua huyo mama akimtafuta mtoto wake?"

225 Sasa, ningezungumza naye kuhusu Bwana, naye angenicheka tu. Nami nikasema, "Bert, unawezaje kufanya hivyo? Unawezaje kamwe kumwua maskini mama huyo?"

226 Sasa, yeye hakuwa mnafiki, hakuwa akijifanya, alikuwa halisi, alizaliwa, kitu fulani ndani yake kilikuwa ni mama, na mtoto mchanga alikuwa hatarini. Naye alikuwa mama, silika ndani yake, silika ya mama, angetembea moja kwa moja mbele ya bunduki hiyo, akijua ya kwamba alikuwa anaenda kufa. Ilileta tofauti gani? Alikuwa akimtafuta mtoto huyo, alikuwa hatarini. Hakuwa akijifanya.

227 Ndipo nikamwona akisawazisha bega hilo chini, loo, jamani, hizo alama za kulenga juu ya moyo huo, Nikawazia, "Yapata sekunde nyingine, ataulipua huo moyo wake mwaminifu hata upande wa pili," risasi hiyo kubwa ya chembe 180 ikitoka pale, nikawaza, "Loo . . ." uyoga, itoboe shimo kama *hilo*. Nami nikawazia, "Yeye ataulipua tu moyo huo mwaminifu wa mama huyo moja kwa moja hadi upande wa pili." Nikawaza, "Anawezaje kuwa katili hivyo?" Nikasema, "Kamwe siwezi kuliangalia."

228 Nikageuza kichwa changu, nikasema, moyoni mwangu nikasema, "Bwana Mungu, naomba umsaidie, usimwache afanye hivyo. Angalia onyesho hilo la umama halisi, angalia kitu hicho halisi."

229 Sasa, mama huyo, akitoka nje moja kwa moja, si mnafiki, si kujifanya, kama washiriki wengi wa kanisa wafanyavyo, wanatenda kana kwamba wao ni Wakristo, wakati shindano la kuamua linapokuja, wanauonea aibu. Alitoka hapo nje moja kwa moja na kitu halisi, akasimama pale na alikuwa tayari kukabiliana na kifo chake. Kwa sababu gani? Ndani yake, alikuwa ni mama, na mtoto mchanga alikuwa hatarini.

230 Nilikuwa nikiomba, nami nikawazia, "Bwana, usimwache afanye hivyo." Nami nikangojea, nikangojea, bunduki haikufyatuka, nikawaza, "Sijui kuna nini?" Nikageuka kuangalia, na mtutu wa bunduki ulikuwa ukienda *hivi*, hiyo mishipa imara ilikuwa imevunjika.

231 Kainyakua bunduki na kuitupa chini, nami nilikuwa nimeketi juu ya chungu ndogo ya theluji namna *hiyo*, akakumbatia miguu ya suruali yangu na kusema, "Billy, nimetosheka nayo. Niongoze kwa Bwana Yesu huyo unayenena habari zake."

232 Ilikuwa ni kitu gani? "Wakinyamaza, miamba itapiga kelele mara moja." Aliona nini? Aliona kitu halisi, aliona kitu ambacho hata asingeweza kuona katika wahudumu wengi ama Wakristo, aliona katika huyo kulungu uaminifu, kitu halisi ambacho kilikuwa halisi. Huyo kulungu alimhubiria mahubiri bora kuliko yote ambayo mhubiri yeyote angeweza kuhubiri. Alikuwa na kitu halisi ambacho angeweza kukishikilia na kujua kulikuwa na umama halisi, na kama kuna umama halisi, kuna Mungu halisi, kuna wokovu halisi. Hapo kwenye chungu hiyo ya theluji, nikamwongoza kwa Bwana Yesu Kristo, naye ni shemasi katika Kanisa la Kwanza la Kibaptisti sasa, Mkristo mwaminifu, kwa sababu aliona kitu ambacho kilikuwa halisi.

233 Ee Mungu, jalia tuwe halisi. Hebu tusiwe na namna fulani ya dini, hebu na tuwe na kitu halisi, ambacho watu wanaweza kuona ya kwamba Mungu anaishi ndani yetu.

Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu.

234 Ninataka kuwaulizeni swali la dhati. Kama mjuavyo vema sasa, ya kwamba mimi—mimi si kasisi, si mnenaji, sina elimu, lakini moyoni mwangu, kuna Kitu fulani ambacho ni halisi, nilimpata Kristo ambaye anamaanisha vile vile kwangu kama yule mtoto wa kulungu alivyomaanisha kwa huyo mama kulungu, Yeye ni zaidi ya maisha yangu, niko tayari kuyatoa wakati wowote. Nami nimemtolea sadaka miaka thelathini na mmoja iliyopita, Anazidi kuwa mtamu siku baada ya siku, kadiri siku zangu zinavyozidi kudhoofika sasa, nami ninazeeka.

235 Kuna mtu hapa alasiri ya leo, ama, ni watu wangapi, niseme, wangetaka kuwa na uhalisi wa Kristo moyoni mwao, kama mama kulungu huyu alivyofanya kwa mtoto wake mchanga? Je, ungependa ukweli huo? Wakati kichwa chako kimeinamishwa, waweza kuinua tu mikono yako, na kusema, "Niombee, Ndugu Branham, ninamtaka Kristo sasa aweke upendo mwingi sana wa kweli moyoni mwangu kwa ajili Yake, kama vile mama kulungu alivyokuwa nao kwa mtoto wake"? Waweza kuinua mkono wako? Useme, "Nikumbuke katika maombi."

236 Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mungu ambariki jamaa huyu mdogo hapa, hapa nje. Loo, huko juu kwenye roshani? Mtu fulani huko juu aseme, "Nikumbuke,

Ndugu Branham, unapoomba." Mungu awabariki huko juu. Hakika, Mungu anaiona mikono yenu, popote mlipo.

237 Mungu ambariki dada huyu aliyeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu. Ubarikiwe, dada mpendwa. Labda ni mama na anajua maana ya umama, nawe unajua jinsi hilo lilivyo aminifu kwa watoto hao, na iwe hivyo kwa Kristo. Atakupa, atakupa huo Roho Wake, Roho Wake Mtakatifu moyoni mwako. Je, ungetaka, mtu mwingine, kuinua tu mkono wako?

238 Unasema, "Hilo lina maana yoyote Ndugu Branham?"

239 Bila shaka, unapita kutoka mautini kuingia Uzimani unapofanya hivyo. "Heri wenye njaa na kiu." Mungu akubariki, ndugu yangu, uliyeketi papa hapa.

240 Kunaweza kuwako na mtu mwingine kabla tu hatujaondoka? Hatutatoa wito wa madhabahuni sasa hivi, la, tunawaomba tu kuinua mikono yenu, kuomba. Tutawaombea wagonjwa.

241 Mungu ambariki msichana huyu, msichana mweusi aliyeketi hapa. Ninii tu, anaonekana kama msichana aliye tu kwenye njia panda za maisha. Mungu akubariki, ewe msichana. Wakati umri huu usiojali wa roki ya utineja, na kadhalika, ukiendelea, ulichukua chaguo la njia sahihi kwa ajili ya Kristo. Mungu na akubariki daima, dada yangu.

Mtu mwingine angesema tu, "Nikumbuke, ndugu, katika maombi. Unapoomba, Mungu na anirehemu"?

242 Mungu akubariki, ndugu yangu, hapa, na yule aliye upande wa pili wa marefu ya kanisa. Naam, Mungu akubariki. Hapo, huyo msichana mdogo huko nyuma, Mungu akubariki, kipenzi. Huyo msichana mdogo, Mungu awe pamoja nawe. Hilo ni zuri sana.

243 Vema. Kuna mwingine anayejua ya kwamba huna upendo wa namna hiyo? Usingeweza kuonyesha uaminifu huo kwa Kristo, ungetaka kuuonyesha, bali hunao. Labda wewe ni mfuasi wa kanisa, isingekudhuru kuinua mkono wako, useme, "Ningependa kuwa nao, Ndugu Branham, ningependa kujisikia moyoni mwangu kuhusu Kristo. . . " Mungu ambariki msichana huyu mdogo aliyeketi hapa. "Ningependa kujisikia moyoni mwangu namna hiyo, kumhusu Kristo kama huyo mama kulungu alivyojisikia kuhusu mtoto wake mchanga." Je, waweza. . .?

244 Kwamba, wakati mtu katili. . .Mungu akubariki huko, naam, upande wa kulia, ninakuona, bwana. Mungu awe pamoja nanyi. Nami nina hakika Yeye hufanya hivyo. Hata shorewanda hawezi kuanguka bila Yeye kujua, anajua mkono wako unapoinuliwa. Anaijua njaa na kiu moyoni mwako, Naye alisema, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana watashibishwa."

245 Je, kunaweza kuwa na mwingine kabla ya maombi? Vema. Mungu akubariki, bwana, naam. Mungu akubariki huko nyuma, naam, Mungu anakuona. Ninangojea tu kidogo, labda wengine wangeinua mkono wao. Kamwe hamtasahau kuinua mikono yenu, nitawahakikishia hilo, kamwe hamtasahau. Labda umelala kwenye barabara kuu mahali fulani ukitokwa na damu, ukisikia gari la kuchukulia wagonjwa likija, damu ikitoka kwenye mishipa yako, unajua umekwisha, utakumbuka uliinua mkono wako. Sivyo, mtu mwingine kabla hatujafunga? Vema, na tuombe.

246 Baba yetu wa Mbinguni aliyebarikiwa, walitoka mashariki na magharibi, kaskazini na kusini kusikia hekima, roho ya upambanuzi iliyokuwa juu ya mtumishi Wako, Sulemani. Na wakati Mwanao, Bwana Yesu, alipokuwa hapa duniani, aliwaambia, jinsi walivyokuwa wamehukumu katika kizazi chao kitu ambacho kizazi cha Sulemani kilikuwa kimethamini sana; na jinsi walivyokuwa wamefanikiwa katika kizazi cha Sulemani, na jinsi ambavyo wangechafuliwa katika kizazi Chake, na hata hivyo Yeye alikuwa mkuu kuliko Sulemani.

247 Na leo, Baba, ni siku kuu kuliko ilivyokuwa siku ile ulipotutembelea hapa duniani katika mwili wa nyama, kwa kuwa katika siku hizo, ule upatanisho halisi ulikuwa bado haujafanywa, Mungu aliishi ndani ya Mtu mmoja, huyo alikuwa ni Mwanawe, Yesu. Na sasa, baada ya upatanisho kufanywa, Kanisa lote lililokombolewa linaweza kumweka Mungu kifuani, Mungu anaweza kuja kifuani mwa Kanisa Lake, na Roho Mtakatifu.

248 Ulisema, "Mkisema neno juu ya Mwana wa Adamu, mtasamehewa," walipokuita Beelzebuli, maana ulikuwa ukiyatambua mawazo ya nia zao. Walipaswa kujua huyo alikuwa ni Roho wa Mungu hapo, alikuwa juu ya Sulemani, juu ya manabii, na hapa alifanywa katika utimilifu Wake ndani Yako. Nao walinena dhidi Yako na kukuita jina baya, wakaiita kazi ya Roho Mtakatifu ibilisi, Nawe ulisema, "Nitawasamehe hilo, bali ajapo Roho Mtakatifu, mkisema neno dhidi Yake, halitasamehewa."

249 Vema, Roho Mtakatifu, baada ya kuwa ndani Yako, kisha akaja juu ya Kanisa, Huyu hapa siku hizi ambaye angekuwa mkuu zaidi wakati huo, kwa sababu Uzima Wako umetia muhuri kazi kwa ajili ya Roho Mtakatifu na kumleta Kanisani, na hata hivyo, "neno dhidi Yake halitasamehewa kamwe." Naye huyu hapa siku hizi, Roho Mtakatifu wa kupendeza, Utu wa Kristo, akisimama miongoni mwetu, akifanya jambo lile lile alilofanya. Kimaandiko kutoka Mwanzo hadi Ufunuo sawasawa na siku za mwisho, alikuwa awe hapa na kufanya mambo haya, naye Huyu hapa. Baba Mungu, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hili!

250 Ninaomba leo ya kwamba kila mmoja wa wale walioinua mkono wao, wakitambua maskini jambo hili rahisi lililotukia, Bwana, kuhusu rafiki yangu mwema, mtumishi Wako sasa, Bert, jinsi ambavyo hilo lilimchukua mtu huyo katili, wakati Wewe hukuwa na mtu yeyote katika nchi hiyo, ilivyoonekana, ambaye angeweza kulifanya, mimi mwenyewe hata nisingeweza kumwongoza Kwako, lakini aliona kitu hicho halisi katika huyo kulungu, zaidi ya alivyoweza kuona ndani yangu, ama mtu mwingine yeyote, lakini Mungu, Wewe ulimwonyesha kwa maskini mama kulungu, naye akamwongoza Kwako, ibariki nafsi yake aminifu, Bwana. Ninaomba leo ya kwamba kupitia kusimuliwa kwa hiyo hadithi rahisi, wengi wameinua mikono yao, wape shauku yao, Bwana.

251 Jalia kwa urahisi wa imani, tunyoshe mikono na kukishika Kiti cha Enzi cha Mungu, na kusema, "Bwana, nimiminie kile kitasa cha dhahabu cha Mafuta ya Roho Mtakatifu wa Mungu moyoni mwangu." Ndipo watakuwa tayari kumfia Kristo, kuonyesha upendo Wake, uaminifu Wake katika karakana yao, nyumbani mwao, katika madhehebu yao, popote pale. Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao. Amina.

252 Mnampenda? Hebu tuimbe tu ubeti mmoja wa ninii wangu, mmoja wa nyimbo za kale ninazozipenda sana, "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Na tunapofanya jambo hili, tutakuwa na ibada ya uponyaji, ama, ibada ya kuwaombea wagonjwa katika muda ki—kidogo tu. Sasa, hebu na tuimbe tu sasa, tuinue mikono yetu. Vema, ndugu.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

253 Sasa, wakati tukiuvumisha mara moja, hili ni kusanyiko lililochanganyikana, Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wapentekoste, hebu, kwa utamu, tuushike tu mkono wa mtu fulani aliyeketi karibu nawe, na kusema, "Mungu akubariki, ndugu, dada," tunapouimba huo tena.

Na . . .
. . . alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

254 Sasa ujumbe umekwisha, mwabuduni tu katika Roho. Paulo alisema, "Nikiimba, nitaimba katika Roho; nikiabudu, nitaabudu katika Roho."

. . . alinipenda kwanza

Hivi hamwupendi huo utamu wa Roho Mtakatifu?

Nampenda, . . . (Limaanishe tu kwa moyo wako
wote.) . . . mpenda,
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

255 Loo, Yeye si ni halisi? Halisi sana mioyoni mwetu, mzuri sana, amejaa rehema sana. Jina Lake Takatifu libarikiwe. Sasa tutafanyiza mstari wa maombi, tuwaombee wagonjwa huku upako huu wa kupendeza . . .

256 Hivi—hivi Neno halikusugui tu kwa namna fulani? Unajisikia vizuri na safi. Ni wangapi wanaojisikia hivyo? Ni kama tu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Imetolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
gharika hiyo,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.
Hupoteza madoa yao yote ya hatia,
Hupoteza ninii yao yote . . . (Hivi hamna furaha
sana kwamba kuna Chemchemi?)
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
gharika hiyo,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

Ah, roho ile ile ya kuabudu!

257 Billy, uligawa kadi za maombi? Uligawa, sivyo? Ngapi? Hamsini hadi mia moja. Ibada yenu ni ya saa ngapi . . . ? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

258 . . . ? . . . ya Mungu huponya. Ukivunja mkono wako, huendi kwa daktari, useme, "Uponye mkono wangu." Unasema, "Urudishe mkono wangu, Daktari." Mungu anauponya.

259 Unasema, "Nina kidole tumbo, Daktari, kikate." Yeye hakuponyi, anaondoa tu hicho kidole tumbo, hawezi kujenga tishu, Mungu hujenga tishu. Hiyo ni kweli? Yeye huponya, Mungu huponya. Si . . .

260 Billy, hivi mama huyo hapo ana kadi ya maombi? Vema, wewe ninii tu—ninii tu—mwache tu abaki, vema. Unaona? Nitamleta hapa juu na kumwombea, kwa dakika moja tu. Sasa, wasemaje? Vema. Kulikuwa na mtu fulani aliyeketi hapa dakika chache zilizopita, angali ameketi hapa.

Vema, hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa dakika moja tu kwa ajili ya maombi.

261 Ee Bwana, saa imekaribia sasa ambapo jambo fulani halina budi kufanywa. Mimi, kwa uaminifu tu nijuavyo, nilileta ujumbe huu mdogo rahisi wa neema na nguvu Zako. Nami nilikuwa nikiwazia kwamba ingekuwa mapema zaidi, nasi tungewaleta watu wanne, watano, kumi na—na Wewe ungemtuma Roho Wako wa upambanuzi, lakini inaonekana, Bwana, ya kwamba—ya

kwamba watu wangetaka tu tuwaombee. Kwa hiyo, mimi... Bwana, labda hivyo ndivyo ulivyoijenga imani yao alasiri ya leo.

262 Kama hiyo ni kweli, Baba, basi nitaomba ya kwamba utanitia mafuta hivyo kwa Roho Mtakatifu, kwamba watu wanapopitia hapa, hawatakuja, wakipitia tu kwa rafiki na ndugu yao, bali watajua ya kwamba anayesimama hapa jukwaani mahali fulani, pasipo kuonekana kwa macho yetu, ni Bwana Yesu kuthibitisha kila Neno ambalo ameandika, yote aliyosema. Lipe kusanyiko imani ya kuamini. Tujalie, Baba. Ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

Tabibu mkuu...
...Yesu mwenye huruma;
Yeye hunena kuuchangamsha moyo wenye huzuni,
Loo, isikieni Sauti ya Yesu.

Ujumbe mtamu sana katika wimbo wa serafi,
Jina tamu kuliko yote katika ulimi wa mwanadamu,
Wimbo mtamu kuliko zote uliowahi kuimbwa,
Yesu, Yesu mbarikiwa.

263 Mpenzi, ulikuwa ni mkutano karibu kama huu, ninamzungumzia mke wangu aliyeketi pale, wakati wote walipokuwa karibu hivi huko Fort Wayne, Indiana, usiku huo, ilikuwa zaidi sana ni ya Wadunkardi, na Waamishi, Wamenoni, na maskini dada mmoja huko nyuma, aliyekuwa akijaribu kumtafuta Roho Mtakatifu, alikuwa, kamwe sitasahau hizo nywele ndefu, nzuri, nyeupe zilizotengenezwa, alikuwa amevaa nguo nyeupe, alikuwa akicheza.

264 Nao walikuwa wakiniletea mtoto mchanga kiwete, nami nikamshika huyo mtoto mchanga mikononi mwangu, nikamwambia huyo mama, "Je, unaamini ya kwamba Bwana Yesu atamponya mtoto huyo mchanga?"

Akasema, "Ninaamini, bwana."

265 Na papo hapo, nikamwombea mtoto huyo mchanga. Nami nikaanza kumrudisha kwa mama, mama akamweka chini, akaanza kukimbia sakafuni, mama akazimia, watu wakaanza kupiga mayowe, ndipo msichana huyo akampokea Roho Mtakatifu, akaruka juu kutoka kwenye piano, nywele zake zikaanguka chini, huku hiyo piano ikiendelea kucheza, "Yule Tabibu mkuu sasa yuko karibu, Yesu mwenye huruma." Huku mamia kadhaa ya watu wamesimama pale wakiangalia hivyo vibao vya pembe za ndovu vikisogea, "Yule Tabibu mkuu sasa yuko karibu."

266 Madhabahu yote imejaa na huku na huko kwenye marefu ya kanisa, na kadhalika, wakilia na kuomboleza, hao Wamenoni, na Waamishi, na kadhalika, wakimjia Bwana Yesu. Hata

wasingeweza, kuomba tena, wakimlilia tu Mungu wapate rehema, waliona kitu halisi. "Yule Tabibu mkuu sasa yuko karibu, Yesu mwenye huruma." Vema.

267 Sasa, bila upambanuzi...Ni wangapi waliopo hapa, walioona huo upambanuzi? Wanaojua habari zake? Inueni mikono yenu, inueni mikono yenu. Loo, hiyo ni kweli. Sasa, mnajua ungeweza kufanywa, lakini kuuombea mstari huu wote, nisingeweza kufanya hivyo. Lakini...

268 Loo, jamani, maskini mtoto huyo mchanga! Mtu yeyote anaweza kuuona uso wa huyo mtoto mchanga. Ni mtoto wako mchanga, dada? Loo, ni huzuni jinsi gani! Njoo hapa, kwa dakika moja tu. Hmm! Nina hakika nyote mtanisamehe. Hebu na tuone hiyo ni nini. Mtafanya hivyo? Huh? Angalieni huyo ni Roho Mtakatifu. Ingekusaidia? Ingekusaidia? Je, ingesaidia kusanyiko? Nilikuwa tu nikisimulia hadithi hiyo ndogo kuhusu yule mvulana mdogo huko Fort Wayne, na halafu kuhusu yule mtoto mchanga. Niangalieni.

269 Sasa, sisemi kwamba...Mnajua ninalomaanisha, kama vile Petro na Yohana walivyopitia kwenye lango liitwalo Zuri, na kumwambia yule mtu kiwete, "Tutazame sisi. Tutazame sisi." Hiyo inamaanisha, "Sikiliza tu yale ninayosema, yazingatie."

270 Basi huyu mtoto mchanga, jambo fulani limetukia, na kama Roho Mtakatifu ataweza kuniambia kuhusu hilo, ingeisaidia imani yako kuamini ya kwamba Yeye angemponya? Vema, ungeamini. Ninajua...Ninagusa sehemu hizo. Nilikuwa nalo hapa si muda mrefu uliopita. Nilikuwa nikishangaa kuhusu kuvuka ng'ambo, nilikuwa na tukio; ninakusudia kulisimulia kanisa juma hili wakati fulani, kile kilichotukia.

271 Sasa, mnajua, mama, kama ningeweza kumsaidia mtoto huyo mchanga, wala nisingefanya hivyo, si—sistahili kuwa nyuma ya Biblia hii hapa. La, bwana. Ningekuwa laghai, hata sipaswi kuruhusiwa kuletwa...kuja nyuma ya mimbara. Lakini kama ningeweza kusaidia, ningesaidia. Lakini jambo pekee ambalo mimi...

272 Kama Yesu alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii aliyonipa, asingeweza kufanya zaidi ya kuwaambia ya kwamba alipokufa pale Kalvari, alinunua uponyaji wa mtoto huyo. Sasa, hawa makasisi wanaweza kukwambia hiyo ni kweli. Hiyo si ni kweli, ndugu? Alifanya hivyo.

273 Basi kama alikuwa amesimama hapa, nawe ungesema, "Loo, Bwana Yesu, utamponya mtoto wangu mchanga, apate afya? Na—na—nakupenda, Bwana, nami nitamlea mtoto huyu akutumikie Wewe, kama tu utamponya mtoto wangu mchanga." Labda amejichoma moto, ama chochote kile, sijui, bali hata iwe nini, "Kama Wewe—kama ukimponya tu mtoto wangu mchanga, nita—nitaahidi nitamlea apate kukutumikia Wewe."

Mbona, Yeye angesema, "Binti yangu, tayari nimemponya mtoto wako mchanga pale Kalvari."

274 Sasa, ungejuaje huyo alikuwa ni Yeye akikwambia hivyo? Vema basi, Yeye angefanya tu kama alivyofanya alipokuwa hapa duniani, angesema, kama yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, mnaona, kitu kama hicho. Mnajua ninalomaanisha? Nikwambie kuhusu huyu mtoto mchanga. Na hiyo ingekusaidia kuamini ya kwamba isingekuwa ni ndugu yako wakati huo, ingekuwa ni Bwana Yesu aliye hapa. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaelewa hilo? Vema. Bwana na asaidie. . .?. . .

275 Dada? Kwa mtoto mchanga? La, si kuungua kwa moto, inaonekana hivyo, bali sivyo ilivyo. Hayo ni matokeo ya baadhi ya matibabu. Madaktari wamefanya yote waliyoweza kwa ajili ya huyu mtoto, lakini ni namna fulani ya ugonjwa wa uvimbe, kama kwamba seli za damu zimesongamana. Nawe umewapelekea madaktari kadhaa, wamemkataa, "Hakuna kitu anachoweza kufanyiwa," walisema.

276 Lakini wewe usiamini hilo, wewe amini ya kwamba Mungu atamjalia mtoto wako mchanga apone. Hiyo ni kweli, ni kweli. Hutoki kwenye mji huu, la. Unaamini unaweza kumrudisha huko Eugene, itakuwa sawa, na Mungu atamponya kwa ajili yako? Unaamini? Unaamini kwa moyo wako wote kwamba Mungu atamponya?

Na tuombe, inamisha kichwa chako.

277 Baba yetu wa Mbinguni, katika nuru ya Kalvari, katika Uwepo wa Roho Mtakatifu, ninamlaani ibilisi huyu ambaye amemfanyia hivi mtoto huyu.

278 Umejificha kutoka kwa daktari, lakini huwezi kujificha kutoka kwa Mungu, toka ndani ya mtoto huyu na umwache mtoto huyu awe mzima! Ninakuamuru kwa kufufuka kwake Yesu Kristo, ambaye Uwepo Wake upo hapa sasa, kwamba usimchafue mtoto huyu tena! Amina.

279 Usitie shaka hata kidogo, kitu kitaondoka usoni mwa mtoto mchanga, imedhaniwa kilikuwa ni alama ya kuzaliwa, kitu kama hicho. Lakini usininii. . .Endelea tu, amini, mtoto atapona.

280 Unaamini sasa kwa moyo wako wote? Vipi kuhusu baadhi yenu huko nje kwenye kusanyiko sasa msio na kadi za maombi? Mnaamini kwa moyo wenu wote? Ili mpate kujua Roho Mtakatifu yupo hapa, iweni na kicho, ombeni.

281 Wewe uliyeketi hapo ukilia, una kitu moyoni mwako, sivyo? Ni mtoto mdogo, pia. Yuko hospitalini huko Portland, ana miguu iliyopindika. Mtoto atafanyiwa upasuaji kesho, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Amini kwa moyo wako wote, mtoto huyo atakuwa mzima. Amina.

282 Aligusa nini? Ninii—ninii yake. . .? Mwulizeni, sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, yeye ni mgeni

kabisa. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako huku na huku, mama. Unaona? Je, kila sehemu ya hayo aliyosema ni kweli? Kama ni kweli, punga wako tena. Simama kwa miguu yako, kama hiyo ni kweli. Hilo hapo.

283 Sasa, unaamini ya kwamba Uwepo wa Kristo upo hapa? Basi amini kwa moyo wako wote sasa, wakati mkiomba pamoja nami. Hatuwezi kukaa muda mrefu sana hapa, tukifanya hivyo, huo utaninii, mwajua, itachukua muda mrefu sana kufanya hivyo. Huo—huo . . . Ni vigumu kuuzuia mara ukishaanza.

284 Huyo mtu aliyeketi hapo ameinua mkono namna *hii*, anaugua kikohozi kiletwacho na vumbi. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Sikujui, sivyo? Hunijui mimi, lakini Mungu anatujua sote wawili. Lakini una kikohozi kiletwacho na vumbi. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Uliwasiliana na nini? Roho wa Mungu. Sasa nenda na uamini, nacho kitakuacha. Kikohozi kiletwacho na vumbi si ugonjwa, ni hali ya pua. Amini tu kwa moyo wako wote, nacho kitakuacha, wala hutakuwa nacho tena, kama ukiamini.

285 Jina la Bwana libarikiwe. Ati mwaniambia ya kwamba Yesu Kristo si yeye yule jana, leo, na hata milele? Hakika ni yeye yule. "Kama unaweza kuamini!" Inaendelea tu kusonga mbele katika kusanyiko. Hebu tuanze tu . . . Kila mtu anisaidie kuomba.

Sasa, bwana, kama sisemi kitu na kukuombea tu, utaamini, sivyo?

286 Bwana Yesu, ninalaani ugonjwa wa mwili wake, na kuombea uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, ndugu.

287 Njoo . . . ? . . . Unajua ya kwamba ninajua shida yako, sivyo? Nisiposema neno, nikuombee tu, utaamini. Wasiwasi umekuacha, kwa hiyo endelea mbele . . . ? . . .

288 Njoo, amini kwa moyo wako wote. Sasa, dada, unatambua ya kwamba Yeye anajua yote kukuhusu. Lakini kama nikikuwekea tu mikono, Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Hebu . . . Njoo.

Baba, ninamwekea mikono, katika Jina la Yesu, jalia apone. Amina.

Sasa, nenda ukimshukuru Bwana, kama tu kwamba tayari imekwisha na kuondoka.

Njoo, dada mpendwa. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na kukupa afya? Njoo, sasa.

289 Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utaondoa kitu hiki kichafu kutoka kwa dada yangu, na jalia aamke asubuhi akiwa mwanamke tofauti. Tujalie, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, nenda ukiamini, dada, usiwe na shaka.

Njoo, ndugu mpendwa, amini kwa moyo wako wote.

290 Bwana wa thamani, ninaomba ya kwamba utamponya ndugu yangu ninapomwekea mikono. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Usiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote.

Unaamini, ndugu? Vema, njoo sasa.

Katika Jina la Bwana Yesu, ndugu yangu na aponywe. Amina.

Ubarikiwe.

291 Hutaki kulemaa maishani mwako mwote, sivyo? Unajua kwamba ninajua shida yako, unaelewa hilo. Kila mtu aliyepita, isingeweza kufichika sasa hata kidogo. Ugonjwa huu wa yabisi kavu utakupata hivi karibuni ikiwa Mungu hakusaidii, bali Yeye atakusaidia sasa. Unaamini hilo?

Bwana Mungu, ninamwamuru ibilisi huyu kwa Jina la Yesu Kristo kwamba atamwacha mwanamke huyu, na jalia aponywe. Amina.

292 Amini. Unaamini? Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Unaona? Hatuwezi kusimama na . . . Mnaona, Roho Mtakatifu . . . Ni vigumu kwangu kujizuia kuwaita. Mara wanapokuja, inaonekana kana kwamba ungelipata, bali huwezi kuwafikia wote. Lakini Roho Mtakatifu yeye yule . . .

293 Unaamini kwamba ninamwamini Mungu? Unaamini hilo? Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Hiyo ni kweli? Basi wewe amini kwa moyo wako wote.

294 Hapa, wewe ndiye mtu anayefuata wa kuombewa? Sikujui, Mungu anakujua. Kama Mungu atanifunulia jambo fulani kukuhusu ambalo unajua silijui, ungeamini kuwa mimi ni mtumishi Wake?

Hilo lingewasaidia huko nje? Mnaona? Vema.

295 Sasa, niangalie tu, na uamini kwa moyo wako wote kwamba Mungu ataniambia jambo fulani kukuhusu ambalo litakusaidia. Unaona? Nawe utajua kama ni kweli ama si kweli, kwa sababu unajua, kitu fulani maishani mwako, ama *kitu kingine* unachokijua, utajua kama hiyo ni kweli ama si kweli, kwa sababu wewe ni shahidi wake.

296 Sikujui, nina shaka kama unanijua au hunijui, isipokuwa iwe ni kwa kunisikia tu, mahali fulani. Lakini sikujui, hakuna njia hata kidogo ya kujua lolote kukuhusu, itabidi ifunuliwe na Roho kama najua habari zako. Hiyo ni kweli?

297 Moja ya shida zako ni ugonjwa wa wasiwasi, una matatizo ya kiroho. Hiyo ni kweli kabisa. Ugonjwa wako wa kimwili ni figo, una moja tu, hilo jingine limekwisha. Hiyo ni kweli. Una

mzigo moyoni mwako, huo ni kwa ajili ya mumeo. Ni sawa kwangu kusema kwamba yeye ni nani? Anakunywa pombe, nawe unamwombea, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa, hiyo ni kweli? Nenda ukaamini sasa, na upokee, katika Jina la Yesu Kristo.

298 Iweni tu na imani, msiwe na shaka, kila mtu aombe. Sasa, Roho Mtakatifu yeye yule yuko hapa vivyo hivyo kila wakati.

Mungu, ninamwamuru adui huyu, katika Jina la Yesu, amwache mtoto huyu mchanga. Amina.

Unaamini sasa, dada mpendwa, atakuwa mzima?

Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Njoo, dada. Sasa, mnajua ya kwamba ninajua shida yenu. Na hebu nikuonyeshe jinsi ninavyojua . . .?. . . kile wewe . . .

Ni watu wangapi huko nje wanaougua ugonjwa wa wasiwasi, wasiwasi tu wa akili, wamefadhaika? Inueni mikono yenu juu.

299 Angalia hapa, unaona, sawa na wako. Sasa, kama unaweza kuponywa ukisimama hapa, wanaweza kuponywa huko nje. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo, kama tu utaamini ya kwamba Uwepo wa Bwana Yesu upo hapa, unaweza kuponywa. Unaamini hilo? Basi nenda ukawe mzima, katika Jina la Yesu Kristo. Amini tu ya kwamba nimekwambia kweli.

300 Vipi kama ningekwambia, uliinua mkono wako chini kule muda mfupi uliopita, ukaponywa? Ungeniamini? Vema, uliponywa. Wakati ulipomkubali Bwana Yesu pale, Yeye alilishughulikia papo hapo. Mungu akubariki.

301 Vema. Sasa, unaugua ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Wengi wao huko nje wanaugua ugonjwa wa moyo. Lakini unaamini ya kwamba Yesu huponya moyo anaoishi ndani yake? Njoo hapa.

Katika Jina la Yesu Kristo, mwanamke huyu na aponywe ugonjwa huu wa moyo. Amina.

Nenda na uamini sasa kwa moyo wako wote.

Njoo, ndugu mpendwa, amini.

Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nenda, usishuku chochote sasa, ndugu, amini kwa moyo wako wote.

302 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, katika Jina la Yesu. Jalia aende na awe mzima. Amina.

Njoo ukiamini. Vema, bwana. Unataka kwenda kula chakula chako cha jioni na kujisikia vizuri juu yake? Basi nenda ukale, katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

303 Kwa nini ni upambanuzi tu? Kumbukeni marafiki, upambanuzi hauponyi. Upambanuzi huninii tu. . . Sauti ya upambanuzi ndiyo inayoponya, mnaona, Sauti ya upambanuzi. Mnaamini hilo?

304 Huh! Umeketi mwishoni mwa safu huko nyuma, shida ya macho yako, na koo lako, na masikio yako. Unaamini Mungu anakuponya? Mwanamume mwenye kitu kidogo chenye milia kwenye shati lake namna *hii*, sikujui, sijawahi kukuona. Lakini kitu fulani kilikugusa papo hapo, sivyo? Nuru hiyo ilionekana moja kwa moja juu ya kichwa chako. Hiyo ndiyo hasa iliyokuwa shida yako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, nenda nyumbani, uwe mzima. Yesu Kristo alikuponya.

305 Sijawahi kumwona mtu huyo. Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba hivyo ndivyo hasa Yesu alivyoangalia kwenye kusanyiko wakati yule mwanamke alipogusa vazi Lake, Naye akasema, "Imani yako imekuokoa"? Hiyo ni kweli? Akapata afya. Mnaona? Vema basi, hivi Biblia inasema kwamba "Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu"? Yeye ni Mungu yeye yule aliyekuja wakati Simoni alipokuja mbele Zake, Naye akasema, "Jina lako ni Simoni"? Je, huyo ni Mungu yeye yule aliyejua jina lake? Unaamini Yeye anajua jambo lile lile, anaweza kufanya jambo lile lile? Unaamini Yeye anajua udhaifu wako?

306 Mnajua ya kwamba Yeye alisema a—aliyatambua mawazo yao; huku si tu kutambua mawazo yao, inasema kile walichokuwa, kile walicho, na kile watakachokuwa. Mnaona? Ina—inafanya zaidi ya hayo, inafunua dhambi. Ni wangapi wameiona ikifunua dhambi, na kuitangaza, na kuwaambia wanaume, kuwaonyesha wanawake wanaoishi nao, na kadhalika? Kama hutaki hilo lifanyike, afadhali ulirekebishe kabla hujaja jukwaani, bila shaka itafanya hivyo.

307 Ni wangapi wamekuwa mikutanoni, inueni mikono yenu sasa, ambao mnaona hilo likifanywa? Inueni mikono yenu, kila mahali. Bila shaka, itaninii, ni kamilifu, Mungu. Wakati mwingine watu wana imani zaidi ya wanavyodhania wanayo. Unajaribu kujifanya kuwa na imani, usifanye hivyo, jinyenyekeze tu.

308 Mtu aliyeketi papo hapo, Nuru ingali iko karibu naye papo hapo. Haikuninii. . . Ilimshangaza, alikuwa na imani kiasi hicho. Hiyo ni kweli. Lakini alikuwa nayo tu. . . Hiyo si ni kweli, bwana? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mtu huyo aliyeponywa papa hapa chini. Hiyo ni kweli. Inashangaza tu, hufikiri unayo. Lakini ni—ni rahisi tu. Amini tu.

309 Hapa, huyu hapa mtu amesimama hapa, sikujui, hiyo ni kweli, wewe hunijui, nadhani, Mungu anakujua. Unanijua kwa kuniona tu kwenye kusanyiko, na mambo kama hayo, lakini hiyo si hivi. Unafikiri kwamba Mungu. . .? Kama angeniambia

kilichokuleta hapa, ama kitu fulani, inge—ingekufanya uwe na imani nyingi ya kuamini? Ingekufanya? Huenda ikakufanya uwe na imani. Vema.

310 Vipi kama ningekwambia ya kwamba—ya kwamba upo hapa kusudi uvimbe huu mdogo uondolewe kichwani mwako hapo? Hilo hasa ndilo lililokuleta hapa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

311 Sasa, kusanyiko huenda likasema, "Hakika, Ndugu Branham, unamwangalia."

312 Vema. Kama huyu ni Roho wa Yesu Kristo, Yeye atamjua huyu mtu, nitawasiliana naye, hiyo ni kweli.

313 Hutoki hapa, kutoka mji unaoitwa Lakeview. Hiyo ni kweli? Wanakuita Bill, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, una imani? Basi nenda ukaponywe, Yesu Kristo anakuponya. Naam, bwana.

314 Mtu yeyote anaona huyu ni mtoto mdogo, anayeteseka. Ninyi nyote inamisheni vichwa vyenu tunapomwombea mtoto huyu mdogo.

315 Papa hapa, si lazima uliseme namna hiyo. Unajua. . . Unaamini ya kwamba Mungu atamchukua maskini jamaa huyu, na kumwondolea huu, na kumwacha apone?

316 Bwana, ninaweka mikono juu yake, katika Jina la Bwana Yesu, namhukumu ibilisi ambaye amemfanyia mtoto huyu uovu. Jalia mtoto arudi hata juma hili na kuonyesha, mama aonyeshe kile kilichomfanyikia mtoto huyo mchanga. Katika Jina la Yesu, ninamkabidhi mikononi mwa Mungu. Amina.

Mungu akubariki, dada. Ninataka kusikia kutoka kwa mtoto huyo juma hili.

Njoo, ewe jamaa mdogo.

Bwana Yesu, mbariki mtoto huyu mdogo na umpe afya, kwa Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, mama, kote. Jina la Bwana lisifiwe.

Njoo, dada mpendwa.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utambariki huyu mwanamke na kumponya, katika Jina la Yesu. Amina.

Iweni na imani, sasa.

Mleteni huyo mvulana mdogo. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kumponya?

317 Baba yetu wa Mbinguni, ninamshikilia mvulana huyu mdogo karibu nami, na kuomba kwamba nguvu za Mwenyezi. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

318 . . .kama si kwa ajili Yako. Ninaomba ya kwamba utamjalia mtoto huyu mdogo aponywe vivyo hivyo, kusudi watu wajue ya kwamba Wewe ni Mungu. Ili mtoto huyu aweze kurudi kwenye

kusanyiko hili kabla mfululizo huu wa ibada haujafungwa juma hili lijalo, na kuonyesha ya kwamba Mungu amemponya, na miguu yake midogo ni mizima, naye anatembea tena.

319 Loo, ewe ibilisi uliyefanya hivi, ninakuapisha kwa Mungu, kwa ufufuo wa Yesu Kristo, ambaye Uwepo Wake upo hapa sasa, mwache mtoto huyu!

320 Pia jalia nguvu za Mungu zichukue mahali pa gango hili, kwamba mtoto huyu atatembea katika nguvu za Roho wa Mungu maishani mwake mwote. Amina.

321 Itakuwa hivyo, bwana? Itakuwa. Mungu akubariki, utapata ulichoomba. Ninakupa mtoto huyo, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

322 Vema? Wewe ndiye mtu anayefuata? Huu ndio mstari wote? Jamaa mdogo kabisa, mimi ni mgeni kwako, sikujui, wewe hunijui, bali Mungu anatujua sote wawili. Kama Bwana ataniambia kilichokuleta hapa, utaamini? Inge—ingekufanya uamini? Ungeamini. Vema.

Ingewasaidia wangapi, hili kusanyiko? Ingesaidia.

323 Kitu cha ajabu kukuhusu, naam. Wewe ni—wewe kwa kweli una—una wasiwasi, umefadhaika, ugonjwa wa wasiwasi. Umetoka mbali sana upate kuombewa. Wewe si—wewe kweli si Mmarekani, wewe ni Mjerumani, umetoka Ujerumani, nawe umekuja hapa kuombewa. Nami naona uliwasili Jeffersonville, nami nilikuwa nimeondoka, nawe umekuja hapa nipate kukuombea, kote kutoka Ujerumani. Ninakurudisha Ujerumani, katika Jina la Yesu Kristo, mtu mwenye afya. Unaniamini mimi?

324 Ninamwondoa mwovu kutoka kwa mtu huyu, katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yake!

325 Jalia awarudie watu wake akiwa mtu mwenye afya, na nitakaporudi kule Ujerumani, Bwana, kwa ajili ya mkutano, jalia kijana huyu awe ushuhuda. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Umeponywa. Rudi nyumbani ukiwa mzima. Auf Wiedersehen.

Bwana asifiwe! Mnaamini?

326 Vipi kukuhusu wewe uliyeketi kwenye hicho kiti cha magurudumu? Unaamini Mungu anaweza kukuponya? Utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Kama ningeweza kukutoa kwenye hicho kiti cha magurudumu, ningefanya hivyo. Siwezi kukutoa, bali Mungu anaweza kukutoa. Kama Mungu atanifunulia sababu yako ya kuketi hapo, utanitii kama nabii Wake? Kansa ikikula kabisa kwenye utumbo. Unanitii mimi kama nabii Wake? Utakufa ukiketi hapo. Huwezi kwenda popote pale. Huenda ukawa dhaifu, kupungukiwa na nguvu, lakini . . .

60-0710 Malkia Wa Sheba
Shule Ya Sekondari Ya Juu Ya Klamath Union
Klamath Falls, Oregon Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org